4 SEPTEMBA, 2026

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Nane – Tarehe 4 Septemba, 2026

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Nne, Kikao cha Nane leo tarehe 4 Septemba, 2026.

Katibu.

NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI Mheshimiwa Sheila Edward Lukuba, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 102

Kulipa Deni la Ujenzi wa Stendi ya Msamvu Morogoro

MHE. SHEILA E. LUKUBA aliuliza:-

Je, lini Serikali itachukua deni la ujenzi wa Stendi ya Msamvu ili kuipunguzia mzigo Manispaa ya Morogoro?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Sheila Edward Lukuba, Mbunge wa Viti Maalumu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro iliingia ubia na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma *(PSSSF)* kwa ajili ya ujenzi na uendelezaji wa Stendi ya Msamvu. Wakati wa ufunguzi wa stendi hiyo, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro iliomba stendi hiyo ikabidhiwe kwa Halmashauri badala ya kuendeshwa kwa ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa *PSSSF* uliridhia maombi hayo na kukabidhi stendi hiyo kwa Halmashauri kwa ajili ya uendeshaji. Hata hivyo, kutokana na malengo ya Sera ya Mfuko wa *PSSSF* ya kulinda michango ya wanachama, Mfuko uliomba urejeshewe shilingi bilioni 20.38 ikiwa ni gharama za ujenzi pamoja na riba. Hivyo tayari Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro imeanza kuchukua hatua za kulipa deni hilo ambapo shilingi bilioni moja zimetengwa katika mwaka wa fedha 2026/2027 kwa ajili ya kulipa deni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua hizo, Serikali inaendelea kufanya tathmini na uchambuzi wa jambo hili ili kuona uhimilivu wa deni la Taifa. Uchambuzi huo utakapokamilika, Serikali itafanya maamuzi kuhusu ulipaji wa deni hilo. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sheila Edward Lukuba.

MHE. SHEILA E. LUKUBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uzinduzi wa Stendi ya Msamvu, Morogoro, ambao ulifanyika tarehe 6/5/2018, sasa ni miaka minane toka Rais aahidi kulipa deni hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri ametoa majibu ya jumla. Je,

lini Serikali inaweza kutoa ahadi kwa tarehe, mwezi na mwaka maalum kukamilisha uchambuzi na kuanza kulipa deni hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nina ombi. Kuna stendi nyingi nchini kwetu hapa zimejengwa kwa fedha ya Serikali, Mfano, kituo cha mabasi Mbezi Luis kule Ubungo, stendi ya mabasi Chato, stendi kuu ya mabasi Dodoma hapa tulipo, kituo cha mabasi Nyegezi na nyingine nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali yangu sikivu chini ya uongozi wa Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ameahidi kuacha tabasamu kwa wananchi wake, kuisaidia Manispaa ya Morogoro kulichukua deni hili na kulilipa. Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ilijenga Stendi ya Msamvu kwa kushirikiana na *PSSSF*, na ni ukweli kwamba Halmashauri hii inakabiliwa na deni kwa ajili ya kurejesha fedha na riba kutokana na uwekezaji wa *PSSSF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwanza tunafahamu, na ndiyo maana hivi sasa Ofisi ya Waziri Mkuu, *TAMISEMI* tunaendelea na mazungumzo na wenzetu wa *PSSSF* ili kuweza kuona namna nzuri zaidi ya kuli-*manage* deni hili ili kuipunguzia mzigo Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro. Kwa hiyo, hiyo ni hatua ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili ambayo tunaendelea nayo ni kufanya tathmini ya deni la Taifa ili kuona uwezekano wa Serikali Kuu kuchukua wajibu wa kulipa deni hilo, ili kuisaidia Manispaa ya Morogoro kuondokana na mzigo wa deni hilo. Kwa hiyo, ni hatua ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya tatu, tunaendelea kusisitiza kwamba kwa kuwa yalikuwa ni makubaliano ya ubia kati ya Manispaa ya Morogoro na *PSSSF*, kwa sasa waendelee

kutenga fedha kwa awamu kama tulivyofanya kwenye mwaka huu wa fedha kwa kutenga shilingi bilioni moja, kuendelea kulipa kidogo kidogo wakati Serikali inaendelea kufanya tathmini. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tu kwamba Serikali inatambua changamoto hiyo na tunaendelea kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ni kweli kwamba Serikali imekuwa ikijenga stendi katika mikoa mbalimbali, dhamira ikiwa ni kusogeza huduma za usafiri na usafirishaji kwa jamii, na tutaendelea kufanya hivyo ikiwemo katika halmashauri ambazo bado hazijapata stendi hizo, ahsante.

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Chiku Athman Issa, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 103

Kutokuwa na Matokeo ya Mikopo ya 10%

MHE. CHIKU A. ISSA aliuliza:-

Je, Serikali haioni kuwa sababu kubwa ya kutokuwa na matokeo makubwa ya mikopo ya 10% tangu ianze ni kukosekana kwa wataalamu wa mafunzo ya biashara?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Chiku Athman Issa, Mbunge wa Viti Maalumu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa sasa imeendelea kutoa mikopo ya 10% kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 na Kanuni zake za mwaka 2024. Sheria na Kanuni zimefafanua utaratibu mzima wa ukopaji, urejeshaji na usimamizi wa mikopo hii ya 10%. Lengo la mikopo hii ni kuwawezesha wajasiriamali kupata

mitaji midogo na ya kati na isiyo na riba kupitia fedha za mapato ya ndani ya halmashauri, ili kuendesha shughuli za ujasiriamali na kurejesha mikopo hiyo ili kuwanufaisha wajasiriamali wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 hadi 2025/2026, jumla ya vikundi vya wajasiriamali 33,594 vikiwemo vikundi vya wanawake 18,580.9, vikundi vya vijana 11,758 na vikundi vya watu wenye ulemavu 3,247 vilinufaika na mikopo ya 10% ambapo kiasi cha shilingi bilioni 357.2 zilikopeshwa kwa vikundi hivyo. Aidha, kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi bilioni 143.43 zilikuwa zimefikia muda wa marejesho na kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 130.04 sawa na 91% zilirejeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utoaji wa mikopo ya 10% kwa wajasiriamali, Serikali imeweka mwongozo wa kuwatumia wataalamu wa fedha, maendeleo ya jamii na wataalamu wengine waliopo katika halmashauri katika kuwaelimisha na kuwasimamia wajasiriamali wanaoomba mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Mwongozo huo umeweka utaratibu wa kutoa mafunzo ya masuala ya fedha na ujasiriamali kwa vikundi vinavyoomba mikopo ili kuwezesha kunufaika na mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuboresha utoaji wa mikopo ya 10% kwa wajasiriamali kwa kuwatumia wataalamu wa mafunzo ya biashara ili kuongeza ufanisi wa mikopo hiyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chiku Athman Issa.

MHE. CHIKU A. ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nilikuwa na swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninataka kujua, je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kuongeza somo la biashara katika mtaala wa masomo ya Maafisa Maendeleo ya Jamii, ili ku-*speed up process* nzima ya kuhakikisha haya makundi maalum yanapata mikopo kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kuondoa sharti la kuwafanya wanufaika waweze kupata mikopo hii kwa makundi ambayo yanakaa mahali pamoja, na pia kufanya biashara ya aina moja? Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Chiku kwa swali zuri, na kwa namna ambavyo ameendelea kuwasemea wananchi wa Mkoa wa Arusha na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimhakikishie tu kwamba Serikali inaona umuhimu wa kuendelea kuboresha mfumo mzima wa utoaji wa mikopo ya 10% ili kuongeza ufanisi kwa wajasiriamali, na tunapokea wazo lake zuri na muhimu na tunafahamu kwamba tunahitaji kuwa na wataalamu, Maafisa Maendeleo ya Jamii, Wahasibu na Watendaji kuwa na *component* ya elimu na mafunzo yanayohusu masuala ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ina dhamira hiyo na tutaendelea kuboresha na kila inapowezekana, kuongeza *component* ya masomo ya biashara kwa wasimamizi. Tutaendelea kufanya hivyo ili tuhakikishe kwamba mikopo hii inatolewa kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kweli kwamba tunafahamu, tunahitaji kuboresha mikopo hii, lakini tunahitaji pia kuwa na vikundi vya wajasiriamali ambavyo vinatumika kama dhamana. Pia zimekuwepo hoja nyingi mbalimbali ambazo zinapendekeza kuondokana na utaratibu wa vikundi, na vilevile kuondokana na utaratibu wa kufanya biashara ya aina moja. Tumeendelea kulisimamia suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vikundi vya watu wenye ulemavu, wanaweza wakakopa bila kuwa na kikundi chochote. Mtu mmoja anaweza akakopa, lakini wanawake na

vijana tunaendelea kulifanyia tathmini ili kuona kama tunaweza tukaboresha kanuni zetu na utaratibu. Mara tukishajiridhisha na ufanisi wa utaratibu huo, tutatoa taarifa rasmi kwa taratibu zetu za Kibunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba siyo lazima kikundi kinachokopa kwa ajili ya kufanya shughuli za ujasiriamali wafanye wote shughuli ya aina moja. Wanaweza wakakopa, lakini wakawa wanafanya shughuli tofauti, lakini mwisho wa siku kinachosimamiwa ni marejesho na ufanisi wa biashara zao, ahsante.

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Buchosa.

Na. 104

Kukamilisha Kituo cha Afya Kata za Nyanzenda na Maisome – Buchosa.

MHE. ERIC J. SHIGONGO aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kata za Nyanzenda na Maisome Jimbo la Buchosa?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Eric Shigongo, Mbunge wa Jimbo la Buchosa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021 hadi kufikia 2022, Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa ilipokea kiasi cha shilingi milioni 750 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Nyanzenda na Maisome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kata ya Nyanzenda ilipokea jumla ya shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya wazazi

pamoja na jengo la upasuaji, na Kata ya Maisome ilipokea jumla ya shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *(OPD),* jengo la wazazi, jengo la upasuaji, jengo la maabara na jengo la kufulia. 90% ya majengo yamekamilika na yanatumika kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kukamilika kwa baadhi ya majengo, bado kuna uhitaji wa miundombinu muhimu ikiwemo jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *(OPD),* jengo la maabara na jengo la kufulia katika Kituo cha Afya Nyanzenda, na jengo la kuhifadhia maiti pamoja na wodi ya kulaza wagonjwa wa Kituo cha Afya cha Maisome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu muhimu katika vituo vya afya vya Nyanzenda na Maisome ili viweze kutoa huduma za upasuaji na za dharura kwa wakina mama, wajawazito na watoto chini ya miaka mitano. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Eric James Shigongo.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, pia ninatoa shukrani nyingi sana kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo inafanyika katika Jimbo la Buchosa, hasa katika sekta ya afya. Sasa ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Kwa Kituo cha Afya cha Nyanzenda, fedha pekee zilizokuja ni shilingi milioni 250 ambazo hazikuweza kukamilisha kituo hiki kiweze kufanya kazi vizuri. Nilikuwa ninaomba kujua, hizi shilingi milioni 250 ili kuona *commitment* ya Serikali, ni lini zitakuja kituo hiki kiweze kukamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa upande wa Kisiwa cha Maisome, Serikali imekamilisha karibu 90% ya ujenzi wa kituo kile, na kwa sasa hivi kinafanya kazi, ingawa siyo *full swing*. Nilikuwa ninapenda kufahamu, hiki ni kisiwa, lakini pamoja na kwamba kituo cha afya kujengwa, bado kuna changamoto ya wagonjwa ikiwemo wakina mama wajawazito kutoka kisiwani

kuja nchi kavu kwa ajili ya huduma za ziada ambazo haziwezekani kutolewa kutoka kwenye kituo kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inaweza pia kufikiria kuwaletea wananchi wa Maisome boti ambayo ni *ambulance* kwa ajili ya wagonjwa, ili kuwatoa kisiwani kuwapeleka kutibiwa katika Zahanati ya Mwangika?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kumpongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Eric James Shigongo. Ni jana tu Mheshimiwa Mbunge aliwaleta Waheshimiwa Madiwani hapa na baadhi ya Wakuu wa Idara Bungeni na walipata kuzungumza na Waheshimiwa Mawaziri wetu na Naibu Mawaziri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Eric Shigongo iko kazi kubwa anayoifanya na Waheshimiwa Madiwani wanamuunga mkono. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la kwanza, Serikali tumeendelea kutenga fedha, na pia tumefanya tathmini ya kutosha Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI vituo 394 ambavyo tutaanza na vile vituo 111 na bajeti yake tumeshaipeleka Hazina. Kwa hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI inaendelea kuratibu na kuhakikisha kwamba tunamalizia miundombinu katika vituo vya afya ili vitoe huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali lake la pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, kwanza ameisemea sana Maisome katika Bunge lako Tukufu lililopita na ameomba sana tuweze kuwajali wananchi wale na kuwapelekea huduma za afya, lakini na leo tena ameleta ombi lingine la kuhusiana na boti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutaendelea kumpa ushirikiano wa dhati na kuendelea kufanikisha zoezi hili. Zipo zile meli ambazo tayari Mheshimiwa Mbunge alizipokea kwa ajili ya huduma nyingine za kijamii, na kwa upande wa boti ya *ambulance*, nimhakikishie kwamba, Ofisi

ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tutaendelea kutafuta fedha na wadau mbalimbali ili kuhakikisha kwamba tunapata boti hii kwa ajili ya wananchi wetu. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, Mbunge wa Viti Maalumu, litaulizwa na Mheshimiwa Yagi Kiaratu.

Na. 105

Ujenzi wa Kituo cha Afya Makanda

MHE. YAGI M. KIARATU K.n.y. MHE. MARTHA N. GWAU aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Makanda Manyoni Mashariki utaanza?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 hadi kufikia 2025/2026, Serikali ilitoa jumla ya shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vitatu vya Chibumagwa, Sanza, Makuru na Kintinku. Vituo hivi vinatoa huduma mpaka sasa. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imetoa jumla ya shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la huduma za wagonjwa wa nje *(OPD)* katika Kituo cha Afya cha Kintinku. Ujenzi umekamilika na jengo litaanza kutoa huduma mwishoni mwa mwezi Septemba mwaka huu wa 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya katika kata za kimkakati zilizokidhi vigezo ikiwemo Kata ya Makanda yenye

wakazi wapatao 13,729 katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yagi Kiaratu.

MHE. YAGI M. KIARATU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Makanda ya iliyoko katika Jimbo la Manyoni ni moja ya kata ambayo iko mbali sana na Hospitali ya Wilaya na haina huduma ya uhakika ya afya. Ninaomba Waziri aipe kipaumbele ili ipate kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Serikali ina mpango wa kujenga *bypass* katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida, na *bypass* hiyo inapita katika kata ya nne, lakini Kata ya Unyamikumbi iko mbali sana na Hospitali ya Wilaya. Pamoja na kuhudumia idadi kubwa ya wananchi katika kata hiyo, lakini pia itatoa huduma baada ya *bypass* hiyo kuanza kufanya kazi. Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga kituo cha afya hapo kwa ajili ya mambo hayo mawili? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Kiaratu Mbunge wa Jimbo la Singida kwa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimjibu maswali yote mawili ya nyongeza kwa pamoja, nianze kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali ni kuhakikisha tunapeleka vituo vya afya na kupunguza umbali kwa wananchi kufuata huduma hasa zile za kwenye hospitali zetu za wilaya ambazo ziko mbali zaidi katika zile kata za pembezoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tutaendelea kumpa ushirikiano wa dhati na ameleta maswali, na sisi tunachukua kama maombi Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kuhakikisha tunaweka kipaumbele katika kukamilisha vituo hivi vya afya na viweze kutoa huduma kwa mama zetu na jamii kwa ujumla, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Sasa tunaendelea na Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana. Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 106

Kuanzisha *Youth Investment Resource Centre*

MHE. HALIMA A. BULEMBO aliuliza:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika kuanzisha *Youth Investment Resources Centre* kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya 2007?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefikia hatua ya kuanzisha kituo cha usaidizi wa upatikanaji wa vifaa, bidhaa na masoko ya nje, *(Youth Investment Resource Centre)* kilichopo Benjamin Mkapa *(SEZ),* Mabibo Dar es Salaam, ambacho kilizinduliwa mwezi Machi, 2026. Kituo hiki kinalenga kutoa huduma za uwekezaji kwa vijana na wajasiriamali mahali pamoja zikiwemo huduma za leseni, vyeti, vibali, usajili wa miradi, utatuzi wa changamoto na kuwaunganisha na rasilimali muhimu za uwekezaji. Hadi tarehe 31 Agosti, 2026, kituo hicho kwa kushirikiana na kampuni ya *Nexa International* kimewezesha jumla ya vijana 44 wakiwemo wanaume 27 na wanawake 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuimarisha na kupanua huduma hizo kupitia programu ya ardhi na viwanda kwa vijana katika maeneo ya Dodoma (Nala), Pwani (Kwala), na Mara (Bunda) pamoja na kusogeza huduma za uwekezaji kwa vijana katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizi zinalenga kuwawezesha vijana kupata rasilimali za uwekezaji zikiwemo ardhi, mitaji, mashine, mitambo, vifaa, malighafi na masoko ili kuongeza uzalishaji, uwekezaji na ajira endelevu kwa vijana. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima Bulembo.

MHE. HALIMA A. BULEMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa fursa hii. Kwa kuzingatia kwamba utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inalenga kuongeza ajira zenye tija, kukuza ujasiriamali na kuwawezesha vijana kushiriki katika shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inaweza kulieleza Bunge kwa takwimu halisi tangu kuanzishwa kwa *Youth Investors Resources Centre* ni vijana wangapi wameweza kupata ajira, mitaji ama kuanzisha biashara hizo? Pia ni vijana wangapi ambao wanaweza kubaki na ajira ama biashara walizoanzisha baada ya miezi 6, 12 mpaka 24?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa idadi ya vijana waliofikiwa siyo kipimo cha mafanikio bila kujua matokeo yao, Serikali ina mfumo gani wa *tracer study* kwa kuthibitisha *survival* ya biashara, uendelevu wa ajira, ongezeko la kipato, na ikiwa takwimu zinaonyesha matokeo hafifu, Serikali iko tayari kuchukua hatua gani mahususi kubadilisha utekelezaji wa programu hii ili uwekezaji wa Serikali uendane na ushahidi na malengo ya Dira 2050? Ninakushukuru.

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti,

nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge Halima Bulembo kwa maswali yake mazuri kabisa yanayolenga kufuatilia kwa ukaribu kabisa maslahi ya vijana katika nchi hii na hasa tukilenga katika utekelezaji wa Dira 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijibu swali lake la kwanza ambalo amehoji kwamba ni vijana wangapi na ajira ngapi ni endelevu? Swali hili ni la kitakwimu, lakini ninaomba kumpa habari njema Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa wakati huu Serikali inaandaa mfumo mahususi ambao utakuwa unapokea taarifa mbalimbali za ajira hizi za vijana na shughuli mbalimbali za ujasiriamali zinazofanywa na vijana na kuziweka katika mfumo mmoja kuzichakata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tayari Serikali imeanza utaratibu wa kufanya *mentorship*. Kwa hiyo, kila kijana anapoanzisha biashara, tayari anakuwa amewekewa utaratibu wa kufanyiwa malezi. Lengo ni kwamba wanapojiajiri vijana hao, wanapofanya uwekezaji, wanapofanya ujasiriamali, ujasiriamali wao uweze kuwa na tija kwa maana ya kuwa endelevu. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba taarifa hizi tutaziandaa, zitahakikiwa ili ziwe ziko sahihi na ataweza kupatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili, na lenyewe lengo lake liko pale pale kuona kwamba kuna uendelevu wa shughuli hizi za kiuchumi ambazo vijana wanazianzisha. Serikali ina mikakati mbalimbali, lakini kubwa kuliko yote ni mkakati wa kufanya *mentorship*, yaani mkakati wa kulea. Kwa hiyo, ulezi unaendelea katika kila *project* hizi za vijana tunazozisikia ambazo kuna mifano mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia *Youth Development Fund* kwenye 10% za mapato ya ndani, kuna zile fedha shilingi bilioni 200 ambazo zimetolewa kwa ajili ya vijana, na fursa nyingine mbalimbali kwenye sekta. Zote hizi kuna *component* muhimu ya malezi ili biashara hizi zisife, ziwe endelevu, na tija ipatikane, vijana wawe wamejiajiri katika namna endelevu. Ninakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zulfa Mmaka Omar, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 107

Program za Mafunzo Kuzalisha Ajira Halisi na Endelevu

MHE. ZULFA MMAKA OMAR aliuliza:-

Je, kuna mikakati gani kuhakikisha kuwa ajira na uwezeshaji wa Vijana haziishii kwenye Programu za mafunzo pekee bali uzalishaji wa ajira halisi?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati mahususi wa Serikali ni kuhakikisha mafunzo kwa vijana yanaendana na mahitaji ya soko la ajira na fursa za uzalishaji, na yanaambatana na mafunzo kwa vitendo, uanagenzi, uzoefu wa kazi pamoja na kuwaunganisha vijana na mitaji, vifaa na zana za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati huu unatekelezwa kupitia programu mbalimbali zikiwemo programu ya kukuza ujuzi, *Build for Better Tomorrow*, *Mining for a Brighter Tomorrow*, programu ya uwezeshaji vijana kiuchumi ya shilingi bilioni 200, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, mikopo ya 10% ya mapato ya ndani ya halmashauri pamoja na programu zinazotekelezwa na *SIDO* na *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, vijana wanaunganishwa na waajiri, taasisi za fedha, wawekezaji, masoko na fursa za ununuzi wa umma ili kuwawezesha kutumia ujuzi waliopata kupata ajira, kujiajiri, kuanzisha na kupanua biashara zao. Ili uwezeshaji huo uzalishe ajira halisi na endelevu, Serikali inaendelea kuhakikisha vijana wanapata ushauri wa kitaalamu, uatamiaji wa biashara, uunganishaji katika minyororo ya thamani na masoko, pamoja na

ufuatiliaji na tathmini ya miradi yao kwa kushirikiana na sekta binafsi na wadau wengine wa maendeleo, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zulfa Mmaka Omar.

MHE. ZULFA MMAKA OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na ninafahamu kwamba na yeye pia ni mdau wa vijana kwa sababu huko ndiko ambako ametokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili. Swali langu la kwanza, ni kuhusu ufuatiliaji na uwajibikaji. Katika majibu ya Mheshimiwa Waziri, nimeona ametaja programu nyingi sana na taasisi nyingi sana. Nami nilipenda kujua, ni taasisi gani hasa inahusika na uwajibikaji huu na ufuatiliaji huu na matokeo ya programu hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, Mheshimiwa Waziri ametaja kuhusu shilingi bilioni 200. Nilikuwa nataka kujua, programu za uwezeshaji vijana kiuchumi kupitia bilioni hizi 200, Mheshimiwa Waziri anaweza kunipatia ni halmashauri ngapi zimenufaika na fedha hizi; ni vijana wangapi; na ni asilimia ngapi tayari zimesharejeshwa na kupatiwa vijana wengine kwa ajili ya kujiendeleza kiuchumi na maisha yao binafsi?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumpongeza Mheshimiwa Zulfa Mmaka kwa maswali yake mazuri sana yanayolenga kufuatilia ustawi wa vijana wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwanza kwa swali lake la kwanza ambalo ameuliza kuhusiana na ufuatiliaji. Ni kweli, kuna fursa nyingi mbalimbali za vijana ambazo ziko katika sekta mbalimbali, ndiyo maana kuna Wizara hii, Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana ambayo kazi yake kubwa inakuwa ni kufanya uratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali inaendelea kufanya hivyo kwa taratibu ambazo zipo kupitia Wizara hii, kwa kushirikiana na Wizara za kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, ni kuhusiana ni kiwango gani katika fedha hii ya programu ya uwezeshaji vijana kiuchumi ya shilingi bilioni 200 ambazo tayari zimetoka na kiwango gani ambazo tayari zimeanza kurudi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hili ni suala la kitakwimu, lakini pamoja na hivyo, takribani shilingi bilioni 54 tayari zimetoka kwenda kwenye makundi mbalimbali ya vijana katika sekta mbalimbali. Pia, ufuatiliaji unafanyika, na takwimu zitaandaliwa na Mheshimiwa Mbunge atafikishiwa ili ziweze kumnufaisha. Ninakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kutoka Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kama kutakuwa na maswali yanayohusu takwimu, ni vema kuwafuata Mawaziri kwa wakati wao ili kupata takwimu sahihi kuliko kuwauliza moja kwa moja hapa inakuwa ni ngumu kuyajua. Hata hivyo, ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa kujibu vizuri.

Tunaendelea sasa na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira. Mheshimiwa Hija Hassan Hija, Mbunge wa Kiwani, aulize swali lake.

Na. 108

Kuongeza Wigo wa Biashara ya Hewa Ukaa *(Carbon)*

MHE. HIJA HASSAN HIJA aliuliza:-

Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kuwawezesha Wananchi kuongeza wigo wa kufanya biashara ya Hewa Ukaa *(carbon)*?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Hija Hassan Hija kutoka Kiwani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni *(NCMC)* imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuwawezesha wananchi kuongeza wigo wa kufanya biashara ya kaboni nchini. Miongoni mwa mikakati hiyo, ni pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa umma na hamasa kuhusu fursa za biashara ya kaboni kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, warsha, semina kwa jamii na makundi maalum na kuboresha mfumo wa usajili wa miradi ya biashara ya kaboni ambapo jumla ya miradi 117 imesajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati mingine ni pamoja na kuendelea kujenga uwezo wa wananchi na jamii kupitia mafunzo na huduma za ushauri, kuunganisha miradi ya kibiashara ya kaboni na masoko ya Kimataifa, kuhamasisha uwekezaji wa ndani kwa kuandaa mikakati na miongozo ya upatikanaji wa fedha ili kuvutia uwekezaji wa ndani katika miradi ya kaboni, na kuweka mifumo ya uwazi ya mgawanyo wa fedha na mikataba ya haki kwa jamii zinazohifadhi misitu na ardhi. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hija Hassan Hija.

MHE. HIJA HASSAN HIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, wananchi wa Jimbo la Kiwani walihamasika sana kupanda miti aina ya mikoko zaidi hekta 120 na kustawi vizuri, je, lini Serikali kupitia Mheshimiwa Waziri itafanya ziara Kiwani kuja kukagua mashamba hayo ya wananchi ili kujiridhisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa biashara hii inahitaji mtaji, utaalamu, na masoko ya Kimataifa, ni vipi wananchi wa Tanzania hasa katika mazingira ya visiwa watafaidika na mfumo huo wa kupata mitaji na elimu ya kaboni?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Hija Hassan Hija Mbunge wa Kiwani kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia masuala ya wananchi wake na hususan kwenye eneo hili la hewa ya ukaa. Vilevile nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wa Kiwani kwa kupanda mikoko hekta 120.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina eneo lenye ustawi wa mikoko la takribani hekta 147,000 na ndiyo maana ninawapongeza kwa sababu wanakuwa sehemu ya hii hazina kubwa tuliyonayo ya mikoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitayajibu maswali yote mawili kwa pamoja. La kwanza, wananchi hawa wa Kiwani watakwenda kunufaika na biashara ya hewa ya ukaa kutokana na mikoko hii ambayo wameipanda. Ninatambua ya kwamba upande wa Zanzibar hatujawa bado na kituo cha uratibu wa hewa ya ukaa lakini Mkurugenzi wa Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ni Mjumbe wa Bodi kwenye kituo chetu cha kuratibu hewa ya ukaa cha Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, nimwelekeze Mtendaji Mkuu wa *NCMC* washirikiane kwa ukaribu na Mkurugenzi wetu wa Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar ili tuweze kuwafikia wananchi hawa wa Kiwani waweze kunufaika na biashara hii ya hewa ya ukaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye eneo hili tunayo maelekezo mahususi kutoka kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipofanya kikao na Wizara yetu ametupa maelekezo kuhakikisha tunaendelea kutoa elimu,

tunasajili miradi, tunatoa huduma za kiushauri na kuhamasisha uwekezaji kwenye eneo hili la hewa ya ukaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, niwahakikishie Wabunge wote kwa maelekezo haya ya Mheshimiwa Makamu wa Rais sisi Wizara tutakwenda kuyasimamia na kuyatekeleza kikamilifu ili wananchi wote wanufaike wakiwemo wananchi wa Kiwani.

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira. Tunaendelea sasa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Salum Khamis Salim, Mbunge wa Bububu, uliza swali lako.

Na. 109

Kuongeza Sehemu za Malisho ya Mifugo

MHE. SALUM KHAMIS SALIM aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kwa Wafugaji pamoja na kuongeza maeneo ya malisho yanayolingana na idadi ya Mifugo?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, ninaomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Salum Khamis Salim, Mbunge wa Bububu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi inaendelea kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu matumizi endelevu ya maeneo ya malisho, uzalishaji na uhifadhi wa malisho, afya ya mifugo, pamoja na matumizi ya teknolojia zinazoongeza tija katika ufugaji. Katika bajeti ya mwaka 2026/2027, Wizara imetenga kiasi cha shilingi bilioni 1.0 kwa ajili ya kuwawezesha Maafisa Ugani kupata mafunzo kuhusu teknolojia na mbinu mpya za uzalishaji wa masoko yatakayowezesha kutoa

elimu kwa wafugaji nchini. Aidha, Wizara imeanzisha kituo cha huduma kwa wateja kwa ajili ya kupokea na kutatua changamoto za wafugaji pamoja na kutoa taarifa, ushauri na elimu kuhusu huduma mbalimbali za mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi na Mamlaka za Serikali za Mitaa, ilitenga jumla ya hekta 196,324.25 katika vijiji 187 na wilaya 22. Hatua hii inalenga kufikia lengo la llani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025 - 2030 la kutenga jumla ya hekta milioni 2.53 ifikapo mwaka 2030 kutoka hekta milioni 3.47 hadi hekta milioni sita ili kukidhi mahitaji ya malisho yanayotokana na ongezeko la idadi ya mifugo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa rai kwa halmashauri zote nchini, wafugaji na wadau wote wa sekta ya mifugo, kusimamia utekelezaji wa mwongozo wa upatikanaji, usimamizi, na uendelezaji wa maeneo ya malisho wa mwaka 2021 unaoelekeza majukumu ya wadau wote wanaohusika katika kuendeleza ardhi iliyotengwa kwa ajili ya malisho katika vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salum Khamis Salim.

MHE. SALUM KHAMIS SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu ya Serikali. Pamoja na Serikali kutenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuwapa mafunzo maafisa ili kuja kutoa elimu kwa wafugaji, je, Serikali ina mpango gani kupeleka mabwawa ya maji, visima, pamoja na majosho karibu na wafugaji?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji mzuri wa mustakabali wa wafugaji wote nchini. Mheshimiwa Mbunge ana swali moja tu la nyongeza, anahitaji

kujua mpango wa Serikali wa kupeleka vyanzo vya maji, visima, na majosho kwa wafugaji wetu sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeendelea kutenga bajeti, na kila tunapopata fedha tunapeleka vyanzo vya maji kwa maana ya mabwawa, tunachimba visima, na pia tunajenga majosho katika maeneo mbalimbali ya wafugaji wetu. Hata hivyo, kupitia Mheshimiwa Rais, Serikali imepeleka magari na vyombo mbalimbali vya uchimbaji wa mabwawa na visima katika mikoa yote ya nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba sana wafugaji wetu nchi nzima waweze kutumia vyombo hivi ambavyo viko katika mikoa yetu, waweze kujichimbia mabwawa na visima, lakini pia nitoe rai kwa halmashauri zetu, kulingana na miongozo yetu, halmashauri pia zinawajibika, kutokana na Waraka Namba Moja wa Rais wa Mwaka 2002, unaoelekeza halmashauri zote kutenga 15% za mapato yote yanayopatikana katika shughuli za ufugaji, kuendeleza vyombo mbalimbali vinavyosaidia kwenye ufugaji ikiwemo kujenga majosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe rai kwa halmashauri zote, kuhakikisha zinatenga hizi 15% na kutumia fedha hizi kuendeleza ujenzi wa majosho na kuboresha vyanzo vya maji katika maeneo yetu ili kusaidia wafugaji na kuboresha uchumi wa wafugaji wetu. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa majibu hayo.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na Wizara ya Katiba na Sheria. Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, Mbunge wa Mbarali, aulize swali lake.

Na. 110

Mabadiliko ya Sheria kwenye Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo

MHE. BAHATI K. NDINGO aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kuchakata na kuleta Bungeni mabadiliko ya Sheria ambazo ni kikwazo katika utekelezaji wa Dira ya Maendeleo?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 17 Julai, 2024 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati akizindua Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, aliielekeza Wizara ya Katiba na Sheria kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Tume ya Marekebisho ya Sheria Tanzania, kuzipitia sheria zote nchini na kupendekeza maboresho ili ziendane na Dira ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imeandaa mpango kazi mahususi wa utekelezaji wa dira ikiwemo kuunda timu za utekelezaji ambapo masuala ya sheria yapo katika kundi la nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa kundi hilo ni Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tume ya Marekebisho ya Sheria Tanzania na Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari timu hiyo imeandaa mpango wa kupitia mifumo 28 ya sheria na kwa sasa timu inaendelea kupitia mifumo ya sheria za viwanda, biashara, uwekezaji, kodi na nishati ili kuhakikisha sheria zilizopo katika mifumo hiyo zinaendana na Dira ya 2050.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo.

MHE. BAHATI K. NDINGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru Serikali kwa majibu mazuri na kwa hatua ambazo wameendelea kuchukua kulingana na kubadilisha sheria zinazoendana na dira yetu ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu ya Serikali, imetuambia kwamba sheria ambazo zimeanza kufanyiwa kazi ni za viwanda, biashara, kodi na uwekezaji. Pia tunafahamu kwamba, miongoni mwa vipaumbele saba vya kwenye Dira yetu ya Maendeleo ya 2050 ni pamoja na rasilimali watu na ustawi wa jamii, kilimo na usalama wa chakula, na mengineyo. Je, maeneo hayo, ni miongoni mwa hizo sheria ambazo zitafanyiwa marekebisho au ni sheria ambazo zinajitosheleza katika utekelezaji wa Dira ya Maendeleo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Tunatambua utekelezaji wa dira umeshaanza na tayari sheria nyingi, bado hazijafika Bungeni. Ni kwa namna gani Dira yetu utekelezaji wake utaathirika kwa kuwa sheria nyingi bado hazijarekebishwa na Dira imeshaanza? Ninakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo kwa maswali yake mazuri sana. Kwa hakika, utekelezaji wa Dira 2050 unahitaji kuwezeshwa kwa mapitio ya sheria mbalimbali ili sheria hizi ambazo ni kikwazo, ziweze kuwa wezeshi, na hasa tukizingatia kwamba utekelezaji wa Dira 2050 tunatarajia 70% ya uwekezaji katika utekelezaji wa dira hiyo utoke katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kama nilivyojibu katika swali hili la msingi, kwamba tayari kazi hiyo ya kufanya mapitio ya sheria imeshaanza, na kuna timu mahususi. Sasa ninaomba niyajumlishe maswali yake yote mawili nijibu kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu hii ambayo inafanya kazi ya mapitio haya ya sheria, ina wataalam kama nilivyotangulia kuwataja, ukiacha kwamba kuna Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tume ya Kurekebisha Sheria na Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, na pia kuna wataalam mahususi kutoka Mipango na watu wa Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachofanyika, wakati tumeanza katika mwaka huu wa bajeti, ni kufanya marekebisho ya sheria; na hizi sheria tumeziweka *in clusters,* katika mifumo. Zile sheria tunazoanza nazo sasa, zimefanyiwa tathmini na kuonekana ni kipaumbele ambazo zitawezesha utekelezaji wa dira ili tusiwe tupo nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali inafanya kazi hiyo kwa umakini, imeainisha, na katika mwaka huu wa bajeti tutakuwa tuna mifumo 12 ya sheria ambazo zitafanyiwa marekebisho ambazo kwa mujibu wa tathmini ni sheria za kipaumbele ambazo zitasaidia kuanza utekelezaji wa dira ili tusikwame, tusiwe tuko nyuma kutokana na sheria kuwa hazijitoshelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hata ile sheria aliyoitaja ya masuala ya kilimo ipo miongoni mwa sheria zitakazopitiwa katika mwaka huu wa bajeti ambayo ni mfumo wa sheria za kilimo. Tunaita Mfumo wa Sheria za Kilimo au Mfumo wa Sheria za Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa maana ni *cluster.* Ni sheria zote zinazodondoka hapo katika sekta hiyo. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuhakikisha inaenda kwa kasi na kwa vipaumbele ili sheria zikae sawa na tusiwe tuna mkwamo katika kuanza kutekeleza Dira yetu ya 2050, ahsante.

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo kwa Mheshimiwa Mbunge kutoka Wizara ya Katiba na Sheria.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Ali Khalil Mirza, Mbunge wa Kiembe Samaki, aulize swali lake.

Na. 111

Kituo cha Polisi Daraja B Wadi ya Shakani

MHE. ALI KHALIL MIRZA aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kujenga Kituo cha Polisi cha Daraja B Wadi ya Shakani ili kuimarisha usalama kuelekea Mashindano ya *AFCON* 2027?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi. Kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Khalil Mirza, Mbunge wa Kiembe Samaki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Jeshi la Polisi inaendelea kuimarisha mkakati wa kusogeza huduma za ulinzi karibu na wananchi kwa kujenga vituo vya Polisi na kuwapanga watendaji kwenye shehia zote nchini. *Ward* ya Shakani kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imehusishwa kwenye mpango wa miaka mitano ya ujenzi na ukarabati unaoanza 2026/2027 hadi mwaka wa fedha wa 2030/2031. Hivyo, ujenzi wa kituo hicho umepangwa kutekelezwa mwaka wa fedha 2029/2030 kwa kuzingatia upatikanaji wa eneo katika *Ward* hiyo. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ali Khalil Mirza.

MHE. ALI KHALIL MIRZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na yanayotia moyo, lakini ninapenda pia kumwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, atakuwa tayari kwenda *site* na mimi baada ya hatua zote za upatikanaji wa eneo kukamilika?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Ali Khalil Mirza kwa jinsi alivyo na hamu na shauku ya kuhakikisha kwamba wananchi wake wanaendelea kubaki katika hali ya utulivu na amani, na pia wakiwa salama, na anavyofuatilia kwa karibu usalama wa wananchi wake kwa kusogeza zaidi huduma za ulinzi katika maeneo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia jitihada zake hizo, niseme tu na nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba endapo atakuwa amepata eneo la kuweza kujenga kituo hicho, basi niko tayari kushirikiana naye kwenda kutembelea eneo husika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali fupi la nyongeza.

MHE. NEEMA G. MWANDABILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika Mji wa Tunduma tuna kituo cha polisi ambacho hakina hadhi ya kuwepo mpakani, kwa maana ya kwamba kinahitaji maboresho makubwa kuweza kujengwa. Swali langu, ninatamani kufahamu, ni lini watatembelea pale katika kile Kituo cha Polisi Tunduma ili waweze kuona umuhimu wa kujenga kituo kipya na cha kisasa katika mpaka ule wa Tunduma? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa hoja yake ya msingi ya hadhi ya kituo cha Polisi na hasa tukilinganisha na eneo lilipo, kwamba ni eneo muhimu kwa sababu ni sehemu ya mpaka kati ya nchi yetu na nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaweka kwenye ratiba yetu wakati tukiendelea na ratiba zetu za mikoa na tutatembelea Kituo cha Polisi Tunduma ili kuona hali yake, na kila litakalohitajika tutalifanya kwa mujibu wa hali ya upatikanaji wa fedha katika bajeti ya Serikali. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Ujenzi. Swali la Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, litaulizwa na Mheshimiwa *Advocate* Edwin Swalle.

Na. 112

Hatua za Haraka za Kukarabati Barabara ya Makambako - Songea

MHE. EDWIN E. SWALLE K.n.y. MHE. DEODATUS P. MWANYIKA aliuliza:-

Je, kuna hatua gani za haraka kuwaondolea wananchi kero inayotokana na kutumia Barabara ya Makambako – Songea ambayo imechakaa?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Makambako hadi Songea yenye urefu wa kilomita 295 umekamilika. Ukarabati wa barabara hii unafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha ambapo kwa sasa kazi zinaendelea kwa sehemu ya Songea - Lutukira kilometa 95. Kwa sehemu zilizobaki za Lutukira – Lwangu kilometa 100 na Lwangu – Makambako kilometa 100, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati, ahsante.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaambiwa ambao tumewasha *mic* zetu tukiwa tunaongea, *Hansard* inarekodi sauti

zetu. Kwa hiyo, ninaomba mkiwasha *mic* msiongee tafadhali. Mheshimiwa Edwin Swalle.

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza, niishukuru sana Serikali kwa kuanza ujenzi wa hii barabara kwa upande wa Songea kwenda Lutukira. Hata hivyo hii barabara, eneo la Makambako kwa maana ya Jimbo la Makambako, na pia Jimbo la Lupembe, eneo la Mtwango, Njombe Mjini yenyewe maeneo yote ya Mjimwema kwenda Kifanya na kadhalika, sehemu nyingi zimeharibika sana na hii barabara imekuwa nyembamba; na wananchi wengi wamekuwa wakipata ajali kwa sababu hii barabara imeharibika na ni nyembamba sana. Wakati Serikali ipo na mpango wa kujenga hii barabara, upi mpango wa muda mfupi wa kufanya matengenezo ya hii barabara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa barabara ya Kibena kwenda Madeke pia ni muhimu sana kwa uchumi wa wananchi wangu wa Jimbo la Lupembe, na Waziri wa Ujenzi aliwahi kuja Lupembe mwaka 2021, akawaahidi kwamba wangejenga kilometa moja Lupembe Barazani wakati ujenzi mkubwa unasubiri mipango ya Serikali, upi mpango wa Serikali wa ujenzi wa hii barabara na ahadi ya kilometa moja kwa Lupembe Barazani? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Swalle, Mbunge wa Lupembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara ya Makambako – Mtwango – Njombe - Songea ni moja ya barabara kongwe za zamani za miaka ya 1984/1985 iliyokamilika, na tunakiri kwamba ni nyembamba na ndiyo maana tumeanza ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea, na hasa yale maeneo ambayo yako hatarishi na ni membamba, Meneja wa Mkoa alishaelekezwa

aendelee kupanua kwenye zile *shoulders* (mabega) ili kufanya yale maeneo ambayo magari yanapata shida kupishana aweze kuendelea kuyapanua wakati tunasubiri mpango mkubwa wa kuikarabati barabara yote. Ndiyo maana tunasema, tusiwekeze sana fedha, tutafanya kwa muda kupunguza hizo ajali kwa sababu tumeshaanza kuikarabati hiyo barabara yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili la barabara ya *Kibena Junction* – Lupembe kwenda Madeke, hiyo barabara imeshasanifiwa yote na tunachosubiri ni kusanifu kwa kipande kile cha kilometa 40. Kilometa ile moja ambayo Mheshimiwa alishaahidiwa, ninadhani atakumbuka alikuja ofisini, akaonana na Waziri na ameshapewa maelekezo Meneja wa Mkoa wa Njombe alete mahitaji kwa ajili ya kile kipande cha kilometa moja pale katika Mji Mdogo wa Lupembe kwa ajili ya kuijenga, asante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Patali Patali, swali la nyongeza.

MHE. PATALI S. PATALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Sisi wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kwa mwaka wa fedha uliopita tuliahidiwa kuanza ujenzi wa barabara ya Mbalizi – Shigamba kwa sehemu kwa kiwango cha lami. Kwa kuwa sasa mwaka wa fedha huu tayari umeshaanza, ninaomba kauli ya Serikali. Ni lini utekelezaji wa ujenzi wa kiwango cha lami wa hii Barabara ya Mbalizi – Shigamba utaanza? Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Patali Patali, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyoitaja ya Mbalizi – Shigamba ni moja ya barabara ambazo zinasubiri kulipwa fedha ya awali *(advance payment)* ili ziweze kuanza kujengwa. Huu ni mwezi wa Tisa mwanzoni, kwa hiyo tuna miezi miwili ambayo tumeshaanza, na tumesema mara kadhaa kwamba Serikali imeshaanza kutoa fedha kwa ajili ya kukwamua ile miradi ambayo bado ilikuwa inasubiri fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika fedha hizo ambazo tunaendelea kuzipokea, moja ya barabara ambazo zinasubiri hiyo fedha ni barabara hiyo ya Mheshimiwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, hizo kilomita 10 ambazo ziko kwenye mpango. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa tumeshaanza kupokea fedha, hiyo nayo ni barabara mojawapo ambayo inapewa umuhimu mkubwa kuanza kupewa hizo fedha ili ianze kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Festo Sanga.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri, leo tunahitimisha Bunge na ninarudi Makete kuongea na wananchi kwa ajili ya barabara ya Mbeya – Makete, na kuna tishio la *El-Nino*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ipi kauli ya Serikali au maelekezo yake kwa *TANROADS* Mkoa wa Njombe kuhakikisha kwamba barabara hii haifungi kwa kipindi hiki kwa sababu ametuhakikishia kwamba fedha zipo na Mfuko wa Barabara umekuwa ukipokea fedha, na sisi Makete tumekuwa na kilio kikubwa? Ipi kauli yako Mheshimiwa Waziri kabla hatujaingia kwenye hatua ya masika, ambapo siyo siku nyingi mvua inaanza? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wizara, tumeshajipanga na Mameneja wote, siyo Mkoa wa Njombe tu, mikoa yote wameshaelekezwa na hasa maeneo ambayo yatakuwa na mvua nyingi ya *El-Nino* wameshajipanga. Kwa Mkoa wa Njombe ambao muda wote una mvua, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa mkandarasi yuko *site*, kwa kawaida anapewa hiyo barabara kuikarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungetamani pia maeneo yote yale ambayo huwa yanakuwa na changamoto yaweze kufanyiwa kazi kabla ya mvua na tunatamani pengine kabla ya kipande cha mvua hata kama kilometa tano mpaka saba ziwe

zimeshapata lami kabisa katika hiyo barabara kabla ya *El-Nino*. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Paschal Chinyele, swali fupi la nyongeza.

MHE. PASCHAL I. CHINYELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Hapa Dodoma kuanzia *roundabout* ya *ring road* pale Bihawana kupitia Nondwa kwenda mpaka Sanza, iko barabara ya vumbi ambayo iwapo pori la Kizigo na Muhesi litafunguliwa, basi barabara hii inaweza ikapitika kwa kilomita 350 kufika katika mpaka wa Tunduma - Nakonde na hivyo kuipunguzia mzigo barabara ya TANZAM, yaani inayotoka Dar es Salaam – Morogoro - Iringa hadi Mbeya. Je, Serikali ina mpango gani wa kufungua hili pori ili nchi iweze kupata barabara nyingine ya kwenda mpakani mwa Tanzania na Zambia? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara kimsingi ni barabara ambayo kwa sasa haipo, lakini ni mapendekezo kwamba tuweze kuifungua. Ni barabara ambayo itapita katika hilo pori kwenda Rungwa ambayo itakuwa ni ya mkato sana kwa watu wa Mbeya, Tabora, Rukwa na hata wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea hilo pendekezo, kama Wizara tulishalipokea, na sasa hivi wanafanya kitu wanaita *reconnaissance survey,* yaani kwenda kuitembelea na kuona uwezekano wa kuifungua hiyo barabara hata kwa kiwango cha changarawe kwanza. Itakapoonekana kweli iko *feasible* kwa ajili ya kuijenga, kwa sababu kama itajengeka itakuwa imepunguza sana umbali kwa watu wanaoenda Katavi, Mbeya na hata Rukwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa, hilo wazo tulishalipokea na kama Wizara tunalifanyia kazi. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Fadhili Ngajilo.

MHE. FADHILI F. NGAJILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza. Swali la

msingi linahusu kero za wananchi. Iringa Mjini kuna kero imedumu miaka 22. Mwaka 2004 wakati wa upanuzi wa Barabara ya Iringa – Dodoma, kuna wananchi walipisha ujenzi wa hii barabara, wako 38. Wananchi 15 tu walilipwa, wananchi 23 hawakulipwa. Hiyo imekuwa kero mpaka leo wamekuwa wakilalamika, na hii inatuharibia hali ya kisiasa. *TANROADS* wamesema hawawatambui hawa wananchi 23, wakati Serikali ya Mtaa inawatambua, Serikali ya Kata inawatambua, hadi Mabalozi wanawatambua. Imekuwaje *TANROADS* wasiwatambue? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kushughulikia mgogoro huu wa miaka 22 ili wananchi wangu wa Kihesa Kilolo waweze kuishi vizuri na kwa amani? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimemwelewa Mheshimiwa Mbunge, hapa ni fidia kwa wananchi ambao walipisha Barabara ya Iringa kuja Dodoma. Watakuwa siyo *TANROADS,* lakini inawezekana ni tafsiri ya sheria kwa wakati huo na wakati wa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, kwamba yawezekana kweli waliondolewa lakini pengine walikuwa ndani ya hifadhi. Kama hivyo ndivyo, kwa sheria yetu, hawawezi kupata fidia, lakini kama barabara iliwafuata ama walikuwa nje ya zile meta 45 kwa wakati huo, wanastahili kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nichukue nafasi hii pia kumwomba Mheshimiwa Mbunge kwa sababu ni suala la miaka 22, baada ya hapa tuweze kuonana, tukutane na wenzetu wa *TANROADS* tujue ni kwa nini hawa watu kama wana haki, wasipate haki yao? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 113

Ujenzi wa Barabara ya Liwale – Nangurukuru kwa Kiwango cha Lami

MHE. ZAINAB R. KAWAWA aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Liwale – Nangurukuru yenye kilometa 231 kwa kiwango cha lami?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Barabara ya Nangukuru – Liwale yenye urefu wa kilometa 231, unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha ambapo kwa sasa kazi za ujenzi zinaendelea kuanzia Kijiji cha Mbuli hadi Liwale kilometa 10. Kwa sehemu iliyobaki Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi. Aidha, Serikali kwa kupitia Programu ya *Contingent Emergency Response Component (CERC)* imekamilisha ujenzi wa madaraja makubwa ya Miguruwe, Zinga na Kimambi katika barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kazi za ujenzi wa madaraja ya Kilongo na Nambunda zinaendelea kupitia dirisha la *Contingent Response Window (CRW)*, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zainab Kawawa.

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea na jitihada ya kukuza miundombinu katika nchi yetu. Pili, ninaipongeza Wizara chini ya Mheshimiwa Waziri wetu *Comrade* Abdallah Ulega, kwa kuendelea kusimamia vyema

sekta hii ya barabara. Tunaona kuna ujenzi wa madaraja kama ambavyo amesema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusu Barabara hii ya Liwale – Nangurukuru, zipo sehemu korofi ambazo zinahitaji matengenezo ya dharura ikiwemo Njinjo, Kipindimbi, na pia kuna sehemu inaitwa Kwa Kinunge pale Ngea; pia kuna sehemu inaitwa Kwa Msauji pale ambapo pamejengwa daraja, na kuna sehemu inaitwa Kwa Bibi (huwa tumezoea kuita kwa Bibi Shusha). Ni maarufu hivyo kwa sababu pana mchanga mwingi sana pale, kwa hiyo magari au mabasi inabidi yasimame watu washuke, ndiyo magari yaendelee na safari; pamoja na maeneo mengine korofi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni upi mkakati wa Serikali wa kutengeneza maeneo hayo korofi ili kusudi barabara hiyo iweze kupitika katika misimu yote ya mwaka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Shughuli zote kubwa za kiuchumi katika Mkoa wetu wa Lindi pamoja na mikoa mingine ya jirani, inategemea sana uimara wa barabara. Tuna barabara ambayo nimeishuhudia inajengwa hii *trunk road* inayotokea Mtwara mpaka Mingoyo kupita Mtama kuelekea Nanganga mpaka Masasi, nimeshuhudia mkandarasi anaendelea na ujenzi katika eneo hilo. Sasa bado barabara ya kutokea Mingoyo kuja mpaka Nangurukuru kuelekea Kibiti mpaka Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha inaanza ujenzi wa barabara hii ya kutokea Mingoyo – Kibiti – Dar es Salaam ambayo kwa sasa hivi ni mbaya sana na tunategemea wawekezaji wa madini kuja katika maeneo yetu kutumia barabara hii, wasafirishaji wa mazao ya ufuta, mazao ya korosho ambayo yote yanalimwa katika Mkoa wetu wa Lindi pamoja na Mkoa wa Mtwara na mikoa mingine ya jirani, na usafiri simenti, usafirishaji wa madini mengine yanayotokea katika mikoa ya jirani hususan Mkoa wa Ruvuma? Barabara hii inahitajika sana, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Kawawa kwa kutambua jitihada kubwa ambazo zinaendelea kufanyika na Serikali hii ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhusu miundombinu na hasa Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Mkoa wa Lindi watakuwa mashahidi kwamba katika kipindi ambacho miundombinu ya Mkoa wa Lindi imefanyiwa kazi, ni katika kipindi hiki cha Awamu ya Sita. Kwa hiyo, hizo pongezi ninaomba nizipokee kwa niaba ya Mheshimiwa Rais, na pia kwa niaba ya Wizara ya Ujenzi kwa niaba ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Nangurukuru – Liwale ni kweli ilikuwa ni changamoto kubwa sana na ndiyo maana imeelekezewa fedha nyingi sana. Tumejenga madaraja matatu makubwa, tayari yamekamilika na mawili yanaenda kujengwa. Bunge hili lilipitisha fedha ya matengenezo ambayo tumeanza kuipokea na moja ya maeneo tumesema siyo tu kujenga barabara, lakini yale maeneo korofi ambayo yanafanya barabara yote iweze kupitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo nimhakikishie Mheshimiwa Kawawa, ni moja ya maeneo ambayo hatutajenga tu barabara, lakini yale maeneo ambayo yanasumbua watu wasiweze kupita. Kwa hiyo, tutakwenda kulifanya hilo katika kipindi hiki cha mwaka huu mpaka awamu hii inakamilika, tutakuwa maeneo tumeshayajenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, swali la pili kuhusu Mingoyo – Lindi – Kibiti – Dar es Salaam, tunakiri kwamba katika barabara ambayo tunasema, ni barabara hizi za *Economical Corridors* kubwa. Moja ya barabara ambayo imeharibika sana ni barabara hiyo ya Mingoyo – Lindi – Kibiti. Mingoyo – Masasi tayari ina wakandarasi wanaijenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichofanyika na ilikuwa ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, kwanza, pamoja na ubovu wake, lakini barabara ipitike. Mtu akianza safari hata kama atachelewa

lakini atafika. Leo hatutegemei mtu akwame kwa sababu ya mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mingoyo – Lindi – Kibiti kwa sababu maeneo yote yalikuwa yanakwamisha yamejengwa madaraja ambayo tuna uhakika hata *El-Nino* inavyokuja, tutakwenda kupita. Habari njema ni kwamba, katika fedha ambayo tunategemea kuipata ya ukarabati, moja ya barabara ambayo ninadhani ni kipaumbele, hiyo Barabara ya Kibiti – Lindi – Mingoyo ipo kwenye mpango wa kupokea fedha za mwanzo kabisa kuanza kuikarabati kwa kiwango kikubwa sana, ahsante.

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kutoka Wizara ya Ujenzi kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge. Sasa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Mecktridis Fratern Mdaku, Mbunge wa Malinyi, aulize swali lake.

Na. 114

Kutekeleza Mradi wa Umwagiliaji Maeneo ya Mtakasisi, Usangule na Sofi – Malinyi

MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutekeleza mradi wa umwagiliaji katika maeneo ya Mkasisi, Usangule na Sofi - Malinyi?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ninaomba nijibu swali Na. 114 kutoka kwa Mheshimiwa Mecktridis Fratern Mdaku, Mbunge wa Malinyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji yanaendelezwa kwa kujengewa miundombinu ya umwagiliaji ya kisasa, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na upembuzi yakinifu na usanifu

wa kina wa Bonde la Usengule lenye ukubwa wa hekta 6,000 linalojumuisha Skimu za Mtimbira hekta 1,800 na Usangule hekta 4,200 ambapo utekelezaji wake umefikia 80%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu hizo, kutawezesha kumwagilia eneo lenye ukubwa wa hekta 52 katika vijiji vinne vya Kalenga Keru, Usangule A, Usangule B na Madibila pamoja na kunufaisha wakulima 5,000. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mecktridis Fratern Mdaku.

MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali yetu, lakini pia ninaomba niulize kwamba, wananchi wa Malinyi wanategemea sana shughuli zao za kilimo. Sasa, Mheshimiwa Waziri amejibu kuhusu Skimu moja tu ya Umwagiliaji ya Usangule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niulize kuwa, Skimu ya Mtakasisi pamoja na Skimu ya Sofi nazo pia zinahitaji ujenzi ili wananchi waweze kuendesha shughuli zao za kilimo. Je, ni lini Skimu ya Usangule kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kuwa imeshaanza upembuzi yakinifu 80%, ni lini wananchi wa Malinyi watarajie kuwa skimu hiyo itakamilika kwa wakati? Pia nini hatima ya Skimu ya Mtakasisi pamoja na Sofi? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kuweka hizi skimu kwenye mpango wa Serikali, ni kuongeza tija, kuwawezesha wakulima kulima zaidi ya mara mbili ili Taifa lijitosheleze kwa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi tunajikita kwenye Dira ya Maendeleo 2020 – 2050 ambayo inalenga Taifa kujitosheleza kwa

chakula. Skimu hizi ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja, za Mkasisi na Sofi ni muhimu kama ilivyo Skimu ya Usangule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hata Roma haijajengwa siku moja, tumeanza na upembuzi yakinifu kwenye skimu hii ambayo inaenda kutoa tija kwa wakulima zaidi ya 5,000 na upembuzi yakinifu umeshafika 80%. Upembuzi huu na jitihada hizi zinaendelea katika maeneo mbalimbali. Tutakapokamilisha na tutakapoanza utekelezaji wa ujenzi wa Skimu ya Usangule, *then* Skimu ya Mkasisi na Sofi tutaziingiza katika mpango wa utekelezaji katika bajeti zitakazokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili, umesema? Nimejibu eeh!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mecktridis, swali la pili uliza kwa ufupi.

MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nina swali moja tu la nyongeza.

MWENYEKITI: Basi ameshajibu tayari. Ahsante sana.

Nilimwona Mheshimiwa Naomy Mwaipopo.

MHE. NAOMY D. MWAIPOPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kuelekea utabiri wa hali ya hewa kwamba mwaka huu pengine tukawa na mvua kubwa za *El-Nino* nchini, Serikali ina mpango gani sasa wa kuandaa mbegu himilivu ili kuepusha hasara kwa wakulima?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejipanga kikamilifu kuhakikisha kwamba tunakuwa na mbegu za kutosha kwa ajili ya ku-*respond* mahitaji ya wakulima na hasa tunapotarajia mvua za *El-Nino* ambazo zinaweza kutatiza suala zima la usambazaji wa mbegu hizi kufikia wakulima kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kupitia Wakala wa Mbegu wa Taifa *(ASA)*, Serikali imeongeza kiwango cha uzalishaji wa mbegu bora, lakini pia kupitia wakala ambaye anasimamia udhibiti wa mbegu *(TOSCI)*, tumekuwa tukihakikisha kwamba wakulima hawa wanapata mbegu bora na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tunaweza kuona kwamba mwaka 2022/2023 tulizalisha mbegu bora kiasi cha tani 64,000, lakini mwaka 2025/2026 Serikali imeweza kuzalisha zaidi ya mbegu bora tani 72,000. Kama nilivyotangulia kusema kwenye swali la msingi, kuelekea Dira ya Maendeleo ya 2020 – 2050, Taifa linaenda kujitosheleza kwa mbegu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kupitia miradi ya barabara vijijini, madaraja ya kisasa, tunaenda kuimarisha usambazaji kupitia sekta binafsi ambao wanakuwa wazalishaji wakuu wa mbegu pamoja na taasisi za Serikali. Kwa hiyo, nimtoe shaka Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba tuna mbegu za kutosha na pia tunasambaza kwa wakati ili wakulima wapate mbegu kwa ajili ya msimu wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Regina Malima.

MHE. DKT. REGINA C. MALIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Ukerewe ina mabonde sita: Bonde la Busegera, Mibungo, Miyogezi, Kiyozu, Busegena na Bugalamila yenye jumla ya ekari 5,210 yanayofaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, lakini mpaka sasa mabonde haya yapo tu, hakuna programu yoyote mahususi ya Serikali ya kuyaendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni umuhimu wa kuyaweka haya mabonde katika Mpango wa Taifa wa Umwagiliaji ili vijana hususan wanaomaliza vyuo vikuu na vyuo vya kati waweze kupata ajira na kufanya maendeleo mbalimbali ya kilimo? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kupitia Bunge lako, nimpe neno la faraja Mheshimiwa Mbunge kwamba, skimu zote ambazo zinafaa kwa ajili ya umwagiliaji, zimeorodheshwa na ziko chini ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mpango siyo matumizi. Ni kwamba tunaenda kwa kadiri tunavyopata fedha kukidhi mahitaji na matakwa ya muda. Ndiyo maana wakati ninajibu swali la msingi, ndani ya Jimbo la Malinyi kulikuwa na skimu tatu ambazo zimetajwa kinagaubaga katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, lakini kwa mwaka huu tumeanza na Skimu moja ya Usangule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la skimu za umwagiliaji, kuna skimu za aina tatu: kuna skimu ndogo ambazo zinamilikiwa na wakulima wenyewe; skimu za kati ambazo zina miundombinu ambayo imeboreshwa ambapo halmashauri pamoja na vyama vya wakulima vinaweza vikashiriki katika ujenzi wa skimu hizo; na kuna skimu kubwa ambayo inasimamiwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge pia ni Mjumbe wa Baraza la Madiwani, tunaomba halmashauri zitenge fedha kwa ajili ya kuendesha skimu za kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo, kwa kuwa malengo ni kushirikisha sekta binafsi katika kuhakikisha Tanzania inaenda kujitegemea kwa chakula, basi sekta binafsi pia ziingie huko ambako bado hatujafika ama hatujapata fedha za kutosha kutekeleza ujenzi wa skimu hizo. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali ya Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa.

Na. 115

Ruzuku ya Mbegu Bora kwa Wakulima

MHE. GEORGE N. MALIMA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaweka ruzuku kwenye bei ya mbegu bora kama ilivyofanya kwenye bei ya mbolea?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ninaomba nijibu swali Na. 115 kutoka kwa Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kupunguza gharama za upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima ikiwemo mbegu bora za mazao mbalimbali kulingana na gharama za pembejeo katika soko, bajeti na vipaumbele kwa msimu husika ili kuwajengea uwezo na kuongeza uzalishaji na tija kwa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msimu wa 2025/2026, Serikali ilitoa ruzuku ya tani 42,898.65 za mbegu bora za mahindi zenye thamani ya ruzuku ya shilingi bilioni 67.69. Jumla ya tani 164 za mbegu bora za mazao ya alizeti, ufuta, mbaazi, choroko, dengu na soya zenye jumla ya thamani ya ruzuku ya shilingi bilioni 1.12. Ruzuku nyingine iliyotolewa ni miche ya parachichi 129,986, korosho 3,200,000, kahawa 30,265,885, kakao 58,190 pamoja na viungo. Katika msimu wa 2026/2027, Serikali itaendelea kutoa mbegu za mazao ya mbaazi, alizeti, ufuta, choroko, dengu, soya, miche bora ya kakao, viungo, parachichi na tufaha. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa George Malima.

MHE. GEORGE N. MALIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, msimu wa mwaka 2025/2026 bei ya mazao ya

chakula kama mahindi, mtama ilikuwa kati ya shilingi 18,000 mpaka shilingi 20,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei hii bado ni kubwa, wananchi wengi wakulima wetu wakiwemo wakulima wa Jimbo la Mpwapwa hawawezi kununua bei hii. Badala yake wameendelea kutumia mbegu za asili ambazo kimsingi hazina tija. Je, Serikali ina mpango gani wa kuendelea kutoa ruzuku hasa kwenye mbegu hizi za chakula ili kuendelea kulinda usalama wa chakula nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Ninaomba niipongeze sana Serikali kwa mikakati mbalimbali ambayo imeendelea nayo inayolenga kupunguza gharama za pembejeo za kilimo hasa mazao haya mbalimbali. Swali langu, je, Serikali ina mkakati gani wa kupambana na mbegu feki ambazo ziko kwenye soko la pembejeo za kilimo hapa Tanzania? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili sijalisikia vizuri.

MWENYEKITI: Rudia kidogo swali la pili kwa sauti kubwa, washa *microphone*.

MHE. GEORGE N. MALIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa mikakati mbalimbali ambayo inalenga kupunguza gharama za upatikanaji wa pembejeo na hasa mbegu bora. Swali langu ni kwamba, je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza tatizo la mbegu feki ambayo limeendelea kuwepo kwenye soko letu la pembejeo hapa nchini?

MWENYEKITI: Sawa, umemwelewa?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K. n. y. WAZIRI WA KILIMO: *Yeah.*

MWENYEKITI: Haya, Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K. n. y. WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya mbegu na pembejeo

hasa mbegu ambazo zinazalishwa na *ASA* na *TARI,* ni mbegu ambazo zina ruzuku ya Serikali, kwa hiyo, hata bei ambayo inaonekana ni kubwa, ingekuwa mara dufu kama Serikali isingeweka mkono wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbegu hizo zote zinazalishwa na Taasisi ya Mbegu *(ASA)* na ndiyo maana zinauzwa kwa bei rafiki ukilinganisha na mbegu ambazo zinazalishwa na taasisi binafsi. Serikali kupitia Wakala wa Mbegu, inaendelea kutoa ruzuku ya mbegu bora ambazo zimethibitishwa ubora, lengo likiwa ni kuongeza tija na kuongeza uzalishaji wa chakula ili kuimarisha usalama wa chakula na kujitegemea katika hifadhi ya chakula na vilevile, kuwasaidia wakulima wapate mbegu bora za uhakika ili waongeze tija katika shughuli zao za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Usimamizi wa Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu *(TOSCI)* tutaendelea kushirikiana na taasisi binafsi na makampuni binafsi kuhakikisha kwamba hakuna mbegu feki ambayo inaingia sokoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara na taasisi kama *FCC,* tunaendelea na tumeshaanza kukamata bidhaa ambazo ni feki. Hata hivyo, kwa kuwa kilimo ndiyo uti wa mgongo, watu ambao wanashiriki kwa nia ovu kuuza bidhaa ambazo ni duni, Mheshimiwa Mbunge ametumia neno feki, hawa ni wahujumu Uchumi, lakini ni wahujumu wa jitihada za Serikali yetu kujitegemea kwa chakula na kumtoa mkulima wetu katika janga la umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, vita dhidi ya bidhaa duni tunaiendesha kwa kasi na yeye tunamwomba ushirikiano kupitia wananchi ambao ni waathirika wa bidhaa hizi duni, atupe ushirikiano ama atupe ushirikiano wa kutujulisha ili tuchukue hatua stahiki kwa ajili ya kujikinga na janga hili. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Joseph Kamonga, nimekuona Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na ninapongeza sana upande wa Serikali kwa majibu mazuri. Kufuatia Serikali kutoa fedha nyingi za ruzuku kwenye mbegu za mahindi na mbolea wananchi wa Ludewa wamepata mahindi mengi sana. Wako wakulima ambao mwananchi mmoja amepata mpaka gunia 10,000 hadi 12,000. Je, Serikali iko tayari kuambana na mimi baada ya Bunge kwisha kwenda kuzungumza na wananchi wale kuona mafanikio yaliyotokana na zao hili la mahindi na kuwasaidia wakulima wale kupata soko? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri. Umemwelewa eeh! Masoko sasa.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na sera nzuri za Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuongeza ruzuku na bajeti ya kilimo, tumeanza kuona matunda ikiwemo mavuno makubwa hususan kule Ludewa na maeneo mengine ya nchi. Tunafahamu kwamba bidhaa inapokuwa nyingi sokoni kuna changamoto ya soko na bei pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejipanga kupitia taasisi zake kama *NFRA* na *COPRA* pia kuangalia uwezekano wa kuziwezesha taasisi hizi kupata fedha na mikopo ambayo ina riba nafuu kutoka kwenye taasisi zetu za fedha ili kuongeza uwezo wake wa kununua mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya Waziri wa Kilimo kwamba ombi lake tumelipokea na tutalifanyia kazi kuongozana naye kwenda kule Jimboni kuangalia changamoto ambayo ipo kuhusiana na soko la mazao ya mahindi. Ninaomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, natoa rai kwa wakulima wa Ludewa, kama tulivyotangulia kusema kwamba kuna janga la *El-Nino,* kwa hiyo, pamoja na kuuza lakini pia watunze chakula ili tupambane na changamoto ambazo zinaweza zikaja kutokana na hili janga la mvua za *El-Nino*. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nami niulize swali dogo la nyongeza. Kwanza tunakubaliana mbegu ni usalama wa chakula na Mungu ametujalia tuna taasisi yetu ya *ASA* inayozalisha mbegu bora ambayo inahimili ukame na mazingira ya nchi yetu na udongo wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ASA* wameingia mikataba mbalimbali na wakulima kwa ajili ya kulima kwenye mashamba yao. Changamoto kubwa, hawalipi kwa wakati. Nini sasa mkakati wa Serikali kuhakikisha wakulima wanalipwa kwa wakati ili wazalishe zaidi tusitegemee tena mbegu za nje ambazo mwisho wa siku ndiyo wanatuletea mbegu feki katika nchi yetu? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Ester Bulaya ambaye pia ni mdau mkubwa wa kilimo kwamba ni nia ya Serikali kujitegemea kwa kuwa na mbegu bora. Pia, ni nia ya Serikali kushirikisha sekta binafsi hasa wazalishaji binafsi katika kushiriki kwenye uzalishaji wa mbegu hizi bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia hilo, taasisi ama Wakala wa Mbegu wa Taifa *(ASA)* imetoa kandarasi ama kuingia mikataba na Watanzania mbalimbali kuzalisha mbegu kwa niaba yao na wao ndio wanunuzi wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya malipo tumeipokea lakini ninamhakikishia kwamba tumeshaanza kuifanyia kazi kwa kupitia madeni yote na tunaenda kuhakiki. Serikali inaenda kuhakiki wale wote ambao wanaidai *ASA* kuangalia uhalali wa madeni hayo na pale ambapo tutajiridhisha na madeni hayo, tutaanza kulipa mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kutoka Wizara ya Kilimo kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tuanze Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo baadaye tutarudi Wizara ya Maji. Mheshimiwa Amina Ali Mzee, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 118

Kuanzishwa kwa *Academy* Maalum ya Kuibua Vipaji

MHE. AMINA ALI MZEE aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha *academy* maalum ili kuibua vipaji kwa watoto kutoka mashuleni?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango wa kujenga shule 56 za michezo nchini na kuhakikisha kila mkoa unakuwa na shule mbili. Kwa sasa tumeanza kwa awamu ya kwanza kwa shule saba na kadri bajeti itakavyozidi kuruhusu, tutaendelea kuongeza, kuhakikisha azma na nia ya Watanzania inatimia kwa kuweka uwezo sawia wa vijana wetu kutumia fursa hii ya kujiendeleza katika fursa ya michezo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Amina Ali Mzee.

MHE. AMINA ALI MZEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri, ninapenda kuipongeza Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mpango mzuri wa kuhakikisha tunajenga shule 56 kwa kila mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutumia vigezo vya kutambua vijana wenye vipaji vya sanaa, michezo, teknolojia ili

kupata fursa sawa? Je, wana mkakati gani kuhakikisha wanawapa mafunzo walimu ambao watakwenda kuwafundisha vijana hawa? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Amina kwa kuendeleza kuweka mkazo mkubwa katika mpango mkakati wa Serikali wa kuongeza utambuzi wa vipaji na ulezi ili kuweza kupata manufaa makubwa ya vijana hawa wanapoweza kupata fursa ya kucheza ndani na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tunao mkakati mkubwa na itakumbukwa kuwa, katika Sera ya Elimu, Toleo la Mwaka 2014 lililotangazwa 2023, uko mpango wa kuwezesha shule zetu za sekondari na msingi kuwatambua vijana ili wapate nafasi ya kushiriki vizuri na kuunganisha na hizi shule maalum tunazozijenga katika mikoa yote tuliyoitaja hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Serikali pia imeruhusu *Private Sector*. Hivi tunavyoongea, tayari tunazo *sports academy* zilizojengwa zaidi ya 204 ikiwa ni fursa nyingine endelevu ya kuwapa *private sectors* kushiriki katika kukuza na kulea vipaji tulivyonavyo katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Amina Ali Mzee ya kwamba Serikali itaendelea, kadri inavyozidi kupata bajeti, kutengeneza mazingira mazuri. Sambamba na hilo, kukuza na kuendeleza vipaji vilivyopo ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utaridhia pia, kupitia nafasi hii ninaomba kulitangazia Bunge lako Tukufu ya kwamba mashindano ya *Miss World* yanayoendelea nchini Vietnam yatafanyika kesho na Tanzania ina mwakilishi aliyekamilika na vigezo vyote, wataanza saa saba mchana na itaisha saa kumi na mbili jioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Habari na Michezo, imewakilishwa na Naibu Waziri wetu, Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, ambaye kuanzia saa kumi na moja na nusu mpaka saa kumi na mbili atakabidhiwa bendera ya kuwa mwenyeji wa mashindano hayo ya *Miss World* Tanzania Mwaka 2027. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Thomas Maganga, nimekuona.

MHE. THOMAS K. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza ninaipongeza Serikali kwa kutoa miongozo ya maeneo mengi kutekeleza *academy* za watoto na kwenye vilabu vyetu kuwa na timu za watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko mengi kwenye *academy* nyingi na vilabu vingi vya watoto, wale watoto wa kwenye zile *Academy* ili wapate namba, lazima waingiliwe kinyume na maumbile na makocha. *Clip* hizo zimekuwa zikitembea sana mitandaoni. Je, Waziri analifahamu hili? Kama analifahamu, Serikali ina mpango gani wa kuchukua hatua maeneo ambayo vitendo hivi vinafanyika? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, swali ni moja tu. Uliza swali moja tu Mheshimiwa Maganga, umeuliza mawili.

MHE. THOMAS K. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa kuna malalamiko mengi kwenye *Academy* na hizi shule za Watoto kwamba ili watoto wapangwe kwenye shule, kwenye hizo *club* za michezo, kuna malalamiko mengi kwamba ili walimu wawapange lazima wawaingilie kinyume cha maumbile, na *clip* zimetembea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kujua, Waziri analihamu hilo? Kama analifahamu, ni hatua gani za kisheria ambazo Wizara imechukua?

MWENYEKITI: Swali ni kwamba Waziri analifahamu ama halifahamu? Swali ni moja tu linatosha. Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Kampala, ambaye amekuwa balozi wetu mwema wa maadili katika nchi yetu ya Tanzania na kila mara tukimsikia tunajua anazungumzia jambo la maadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili alilolizungumzia kwa kweli ni jambo la maadili kwa sababu kijana mwenye kipaji hapaswi kulipa au kutozwa fedha ili acheze. Kipaji chake ndiyo kinapaswa kutumika kama kigezo cha kumpanga na kumpa fursa ya kucheza. Serikali inafuatilia na tumetoa maelekezo mara kwa mara na tunajua vyombo vya Serikali vipo na tutahakikisha ya kwamba kazi hiyo inafanyika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakupa mfano mmoja mdogo tu. Mechi ya Simba na Yanga ambayo huwa inafanyika Zanzibar kwenye Uwanja wa Amani, kwenye *collection* ya mapato tulikuwa tunapata shilingi milioni 40, lakini maelekezo ya Wizara tulivyoyatoa mwaka huu, mechi imechezwa kwenye uwanja ule ule, tumepata takribani ya shilingi milioni 217. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unaweza ukaona matendo ya maadili haya hayako tu kwenye upande mmoja wa namba, lakini hata kwenye *collection,* kwenye *attitude* ya watu kupata fursa kwenye usajili. Kwa hiyo, Serikali inaendelea kuweka mikakati thabiti ya kupanga na kuhakikisha kwamba tunaweka macho yetu yote ili tuwapate watu wenye vipaji na ndani ya vile vipaji, fedha ipatikane na Taifa liweze kunufaika. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nimekuona Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kutambua kazi kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara katika kuendeleza hii Wizara ya Michezo na hasa katika ujenzi na uboreshaji wa viwanja vya *AFCON,* wananchi wa Wilaya ya Hanang wameamua kuunga mkono jitihada za Serikali na kuamua kutenga fedha katika halmashauri yetu, na tayari

tumeshajenga uwanja wa kisasa na hasa tukizingatia Wilaya ya Hanang ndiyo kitovu cha mchezo wa riadha. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuambatana na mimi kwenda kuona jitihada kubwa zilizofanywa na wananchi wa Hanang katika kuhakikisha wanaendeleza na kupongeza kazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge Asia kwa kazi nzuri wanayoifanya wananchi wa Jimbo la Hanang pamoja na uongozi mzima. Pia, kupitia fursa hii, niruhusu niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamefanya jitihada mbalimbali na kuhakikisha kwamba wanachochea maendeleo ya michezo kwa kujenga viwanja, kwa kuwa na ligi mbalimbali ndani ya majimbo yao pamoja na kuendeleza kuunganisha nguvu na Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia tu Mheshimiwa Asia kwamba Wizara yetu tuko tayari. Mimi binafsi, niko tayari kutembelea na kwenda kuwaunga mkono ndugu zangu wa Hanang, na pia kwenye maeneo mengine mbalimbali ikiwemo na kwa kaka yangu kule Sengerema ambako naona uwanja unajengwa kwa kasi kubwa ikiwa ni ishara njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazo taarifa pia kutoka Kibaha kwa ndugu yangu Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, kwa kweli ninawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuendeleza gurudumu hili la kumuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ndio mchezaji namba moja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa tunakwenda Wizara ya Maji, Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 116

Kutatua Kero ya Maji Kata ya Lihimalyao – Kilwa

MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kutatua kero ya maji katika Kata ya Lihimalyao – Kilwa wakati wakisubiri upanuzi wa mradi wa Pande *Plot*?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed, Mbunge wa Viti Maluum, Mkoa wa Lindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha inafikisha huduma ya majisafi na salama kwenye maeneo yote nchini ikiwemo Kata ya Lihimalyao iliyopo katika Wilaya ya Kilwa, Mkoa wa Lindi. Kata hiyo ina jumla ya vijiji sita vya Lihimalyao Kusini, Lihimalyao Kaskazini, Namakongoro, Kisongo, Ruyaya na Rushungi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji viwili vya Ruyaya na Rushungi vinapata huduma ya maji kupitia miradi iliyojengwa na Serikali katika maeneo hayo wakati uchimbaji wa kisima katika Kijiji cha Kisongo ukiwa umekamilika na ujenzi wa miundombinu ya kutoa huduma ya maji utafanyika katika mwaka huu wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kupitia bajeti ya mwaka huu wa fedha 2026/2027, Serikali itachimba visima na kujenga miundombinu rahisi ya kutolea huduma ya maji kwa wananchi wa vijiji vitatu vya Lihimalyao Kusini, Lihimalyao Kaskazini na Namakongoro kupitia mpango maalum wa kufikisha huduma ya maji kwenye vijiji 1,575 visivyo na huduma hiyo kote nchini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed.

MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikiri wazi ya kwamba mimi pamoja na wananchi wenzangu wa Lindi tunatambua kwamba Serikali inayo dhamira ya dhati kuhakikisha kila Mtanzania anapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubaliane na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, ni kweli vijiji vitatu vimechimbwa visima. Niliwahi kueleza hapa Bungeni kwamba maji yale ambayo yanapatikana ni maji yenye chumvi kali sana ambayo hayafai kwa matumizi ya binadamu. Mpango ulikuwa kutoa maji kutoka Kata ya Pande ambayo ni kata jirani na kuleta Kata ya Lihimalyao. Kwa hiyo, ningetamani kufahamu, je, mpango huu wa kutoa maji baridi kutoka Kata ya Pande kuleta Lihimalyao utaweza kukamilika lini na nini ambacho kinakwamisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Ninaishukuru Serikali, kama alivyosema kwamba mwaka huu wa fedha kimetengwa kiasi cha fedha kwa ajili ya kuchimba visima au kuleta maji katika vijiji vya Lihimalyao Kaskazini, Kusini pamoja na Kijiji cha Namakongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetamani sana Mheshimiwa Waziri atupatie *timeframe* tujue ni lini wananchi hawa watapata maji safi na salama kwa sababu wananchi hawa wanakunywa maji ya kwenye madimbwi yanayobaki mvua zinaponyesha. Maji yanapokauka wanatembea umbali wa kilomita sita mpaka saba kwenye mapango kwa ajili ya kutafuta maji. Kwa hiyo, ningetamani Mheshimiwa Waziri aseme neno lake ambalo litakata hamu yangu ya kuona wananchi wa Kata ya Lihimalyao wanapata maji safi na salama. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu maswali mazuri kabisa ya Mheshimiwa Kijakazi, Binti Lindi kwa niaba ya wananchi wa Kilwa. Kwanza kabisa nikiri kwamba Mheshimiwa Kijakazi alishauliza swali hili, lakini katika swali la nyongeza. Alivyoliuliza na mimi kwa niaba ya Serikali nilikubaliana naye kabisa, pasipo shaka. Eneo lile hata kama tukienda

kubadilisha eneo la kuchimba kisima eneo lingine ndani ya kijiji kile bado yatakayopatikana yatakuwa na chumvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilivyomjibu kipindi kile nitamjibu leo hivyo hivyo. Kwa bahati nzuri leo sasa tunalijibu likiwa tayari tumeliwekwa kwenye mpango wa bajeti kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaenda kutumia mradi wa *Pande Plot* ambayo ni maji baridi ya kutosha, hayana shaka kabisa, yataweza kufika katika eneo ambalo lina maji ambayo siyo rafiki kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimtoe hofu kwa sababu bajeti hii ni ya wananchi, na Mheshimiwa Rais ameshaelekeza kwamba tuanze haraka sana mchakato wa utekelezaji kuhakikisha mradi huu sasa tunaenda, badala ya kuchimba visima, ile fedha ambayo ilikuwa imepangwa kwenda kuchimba visima na kuendeleza miundombinu rahisi ndiyo ambayo tunaenda kuibadilisha, inaenda kuvuta, kuleta mabomba, kuleta katika eneo ambalo lina changamoto ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimtoe hofu kwamba hili tunaenda kulifanyia kazi kama ambavyo dada yangu Mheshimiwa Kijakazi Binti Lindi ambavyo ameendelea kuwapigania wananchi wa Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *time frame*, inaendana na hatua za kumpata mkandarasi. Baada ya kumpata mkandarasi, ndipo sasa kulingana na *detailed design* ambayo itakuwa imefanyika na kubaini kwamba mradi huu utakamilika kwa muda gani, nitaweza kumpatia majibu ya uhakika baada ya zoezi hilo kuwa limekamilika, lakini itakuwa ndani ya bajeti ya fedha ya mwaka 2026/2027 mradi huo utaenda kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Agnesta Kaiza.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami kwa mara nyingine niweze kuuliza swali la nyongeza. Ninatambua jitihada nzuri na kubwa za Serikali chini ya Wizara ya Maji za kumtua mwanamke ndoo kichwani na wananchi wote kwa ujumla. Jitihada hizi za kumtua mwanamke ndoo kichwani hazijaleta matunda kabisa ndani ya Jimbo la Segerea. Leo ninadhani ni mara ya sita ninaulizia suala hili la ukosefu wa maji safi na salama. Uzuri Mheshimiwa Naibu Waziri anaishi ndani ya jimbo langu, hivyo anafahamu changamoto ya maji ndani ya Jimbo la Segerea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kufahamu, na leo tunakwenda kuahirisha Bunge, wananchi wa Jimbo la Segerea, hawapati maji kabisa, tunaishi kwa kutumia maji ya mgao. Huo mgao, hatupati kabisa. Kupitia Bunge hili Tukufu, nitumie nafasi hii kwanza kumshukuru sana *DC* wetu, kaka yangu Edward Mpogolo kwa sababu amegeuka kuwa kama *DAWASA* ndani ya Jimbo la Segerea akisaidiana na meneja, kwenda kuwatuliza wananchi kila kata, kila mtaa kwa sababu hawapati maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefikia sehemu wananchi wanatumia maji machafu ya kwenye mashimo. Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaporudi jimboni leo, na uzuri siku ya leo wapo watendaji wa kata 13 zote za Jimbo la Segerea, wanasikiliza kauli yake leo, je, ni kweli kwamba jitihada hizi zimeshindikana kuleta matokeo ndani ya Jimbo la Segerea? Ninaomba majibu ya Naibu Waziri. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kwa hisia kali ambazo Mheshimiwa Mbunge amezionesha, na kwa yale aliyoyatamka, mimi ninakubaliana naye kwa asilimia kubwa. Ni kweli kabisa Segerea maji yanapatikana kwa mgao. Hili linaenda sambamba na maeneo ya Kibamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Jiji la Dar es Salaam eneo ambalo linaongoza kwa kuwa na changamoto kubwa sana ya maji ni Jimbo la Segerea. Mimi ninakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kusema kwamba Jimbo la Segerea upatikanaji wa maji siyo kwamba maji hakuna kabisa, maji yapo isipokuwa kulingana na ongezeko kubwa la wananchi katika Jimbo la Segerea, ndiyo inayosababisha uzalishaji kuzidiwa na mahitaji yaliyopo, na sasa Serikali tumeliona hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokifanya, tunaenda kuweka mpango wa muda mrefu, kwa sababu haya ambayo Mheshimiwa Mbunge alishaulizia kuhusu kuongeza uzalishaji, kuweka *pump* ambayo ilikuwa imeharibika, hii ni kuleta *consistency* tu ya ule mgao uweze kuendelea kwa namna ile ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunachotaka kufanya Serikali, siyo kuleta *consistency* kwamba watu waendelee kupata mgao, tunataka kuongeza uzalishaji ili wananchi wa Segerea wasiwe na mgao ambao unawaumiza sana, hata katika biashara zao. Huo ndiyo uelekeo wa Serikali. Nimtoe hofu kwamba tunayo nia ya dhati kabisa na Serikali imejipanga kwa sababu Mheshimiwa Agnes alitupitishia bajeti yetu kwa kishindo. Ninamhakikishia, hatutamwacha katika hili, tutatembea pamoja kuhakikisha kwamba tunaenda kutatua changamoto ya maji katika Jimbo la Segerea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie, katika kipindi hiki cha Mkutano wa Bunge ambao leo unaisha, ninaomba tuonane ili tushirikishane katika mipango ambayo tunaanza kuiandaa kwa ajili ya Jimbo la Segerea, katika kuhakikisha wananchi wake wasiwe wanaona kwamba hawasikiki katika Bunge wakati anaongea na sisi Serikali tunasikia. Nimtoe wasiwasi kwamba Serikali hii iko makini na maelekezo ya Mheshimiwa Rais yako wazi kabisa, na dhamira ya Serikali yake iko makini, ni kutatua changamoto za wananchi. Sisi tupo tayari kwenda kuitatua changamoto hiyo. Ninakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Christina Mndeme.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Wilaya

ya Kilolo ni kati ya wilaya ambayo kwa kweli bado changamoto ya maji ipo. Tumeshachimbiwa visima, kwa mfano Kata ya Ruaha Mbuyuni bado hawajakamilisha. Tunao mradi wa Kata ya Ng'ang'ange ambao tayari ujenzi wake umefikia 85%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini sasa mkandarasi atapatiwa fedha ili mradi uweze kufanya kazi kwa sababu wananchi wameusubiri kwa muda mrefu sana?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa Ng'ang'ange ninaujua vizuri sana. Kwa bahati nzuri nikiwepo na Mheshimiwa Mbunge, nilishuhudia utiaji saini wa mkataba huu wakati unaanza. Huu mradi ulikaa kwa muda mrefu bila hata kuanza. Leo Mheshimiwa Mbunge mwenyewe anakiri kwamba mradi sasa umeshaanza na umefikia 85% na Serikali tayari ilikwishamlipa mkandarasi kiasi cha kuanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu kwa sababu sasa tumeanza kupata mtiririko mzuri wa kifedha. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mkandarasi huyu tunaenda kuendelea kumlipa fedha, ili aendelee kuhakikisha kwamba mradi unakamilika kwa wakati na wananchi wa Kilolo katika Jimbo la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, wapate huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ambapo kutaonekana kuna changamoto ya ucheleweshaji, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge nitaendelea kumpa ushirikiano kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, ili tuhakikishe mradi huu unakamilika na uanze kutoa matokeo yaliyotarajiwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nilimtaja Mheshimiwa Christina Mndeme, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Lukumay.

MHE. CHRISTINA S. MNDEME: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa hii. Kwa kuwa Serikali imekuwa ikifanya kazi nzuri ya kuhakikisha kwamba huduma za maji zinawafikia wananchi, ikiwemo katika vituo vya afya, zahanati na

hospitali, na kwa kuwa, baadhi ya vituo vya afya na zahanati ndani ya Mkoa wa Tabora bado hazijafikiwa na huduma hiyo ya maji, je, Serikali ina mpango gani na lini itapeleka maji na kutatua kero ya upatikanaji wa maji katika Kituo cha Afya cha Ilolangulu kilichopo Wilaya ya Uyui na hivyo kuwaondolea adha na changamoto hasa wanawake na watoto ambao wanakwenda kupata huduma katika Kituo cha Afya cha Ilolangulu? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni afya, maji ni uhai, maji ni sehemu ya elimu. Nimpongeze sana mama yangu kwa kuendelea kuwapigania wakina mama wa Tabora. Unapogusa katika vituo vya afya, umewagusa watoto, umewagusa wajawazito, umewagusa wazee wa zaidi ya miaka 60 wasioweza kujitegemea kupata huduma nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, ninapenda kusema kwamba Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, alitoa maelekezo. Maelekezo haya yalitolewa kwenye ofisi yake, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Wizara ya Maji na sasa Makatibu Wakuu wamekaa chini na kuanza kufanya tathmini ya taasisi zote za umma, shule za msingi, sekondari, zahanati, vituo vya afya, ili kuweza kubaini mahitaji halisi ili kuweka mkakati wa kwenda kutekeleza agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu ili Watanzania wasipate shida wanapofika katika huduma za afya, wanapohitaji huduma ambayo inahitaji kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Serikali tunaendelea kuipokea na tutaharakisha kuhakikisha utekelezaji wake unaanza mara moja. Nimtoe hofu kwa kufanya hivyo, maeneo ya Uyui ambayo Mheshimiwa anayasemea, Sikonge, Urambo, Kaliua, na huko Ulyankulu, Igunga na Nzega, ninamhakikishia kwamba tutavipa kipaumbele vituo vyote ambavyo viko katika eneo lake ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Tabora wanapata huduma iliyokusudiwa kama ambavyo Mheshimiwa Rais aliahidi kwa Watanzania. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Lukumay, nilikutaja, swali fupi la nyongeza.

MHE. DKT. JOHANNES L. LUKUMAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza kwa Serikali. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Mhandisi Kundo Mathew kwa ufuatiliaji wenye tija wa miradi ya maji katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Arumeru Magharibi, kuna mradi mkubwa wa shilingi bilioni 520, unaopeleka maji katika Jiji la Arusha. Niliomba Serikali isaidie kata zilizo karibu na mradi huo nao wapate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge, na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutembelea jimbo langu, tukamweleza matatizo haya, akafikisha kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hatimaye tukapata shilingi bilioni 2.7 ya kununua mabomba kusambaza katika kata hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba kufahamu, je, ni lini Serikali itapeleka mabomba na kusambaza katika Kata ya Sambasha, Kimnyaki, Olorien, Tarakwa, Kiranyi, ili wananchi wenye imani kubwa na Serikali yao sikivu waende wakapate maji hivi sasa? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, na ninamshukuru sana kaka yangu kwa swali lake zuri ambalo linalenga kuwatetea wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, suala la Mheshimiwa Mbunge ni la kisera. Mradi unatoka Moshi, unapita kwenye jimbo lake unaenda mpaka Arusha Mjini, na sasa tunafanya *extension* mpaka kwenda Monduli kule. Maji yametoka Moshi, kule Hai kwa Mheshimiwa Saasisha Mafuwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusu maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, hayo hayana mjadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, tumeweka kwenye bajeti shilingi bilioni 2.7 kwa ajili ya kwenda kutekeleza mradi huo, kazi imeisha. Kazi iliyobaki sasa tunachosubiri ni kwamba, wazalishaji wa mabomba kwa sasa inavyoonekana ni kama vile kuna changamoto fulani ya *materials* ambayo wanatumia kuzalisha mabomba. Kwa hiyo, *queue* imekuwa kubwa sana katika kusubiri yale mabomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaweka msukumo ili kuhakikisha mabomba ambayo yanatakiwa kwenda katika jimbo lake yanapatikana na yanakwenda kulazwa ili yaweze kutoa huduma kwa wananchi ambao wamekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba sera yetu ni kilometa 13 kulia, kilometa 13 kushoto. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba maeneo ambayo miundombinu inapita, wananchi wasiwe sehemu ya kushuhudia kwamba maji yanapita, wawe sehemu ya kuyaishi maji, wawe sehemu ya kuyatumia maji na waweze kunufaika na rasilimali za Taifa lao.

MWENYEKITI: Mheshimiwa tunamalizia swali la Wizara ya Maji kutoka kwa Mheshimiwa Adonis Alfred Bitegeko, Mbunge wa Muleba Kaskazini.

Na. 117

Ujenzi wa Miradi ya Maji ya Makongora na Iroba Muleba Kaskazini

MHE. ADONIS A. BITEGEKO aliuliza:-

Je, lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa Miradi miwili ya Maji ya Makongora na Iroba katika Jimbo la Muleba Kaskazini ili kutatua tatizo kubwa la maji?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Adonis Alfred Bitegeko, Mbunge wa Muleba Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imepanga kutekeleza mradi wa maji Makongora sambamba na ukarabati wa skimu ya maji ya Iroba katika Wilaya ya Muleba Mkoani Kagera. Kwa pamoja miradi hiyo itagharimu zaidi ya shilingi bilioni 1.84, ambapo miongoni mwa kazi zinazotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa chanzo cha maji, ujenzi wa nyumba ya mitambo *(pump house),* ujenzi wa matanki mawili ya ujazo wa lita 225,000, ulazaji wa mabomba umbali wa kilomita 12.8, sanjari na ujenzi wa vituo 24 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo ikikamilika, itanufaisha zaidi ya wananchi 8,040 waishio katika vijiji viwili vya Makongora pamoja na Iloba, vilivyopo Jimbo la Muleba Kaskazini Wilayani Muleba, Mkoa wa Kagera. Ninakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Adonis.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunashukuru sana na tunawapongeza Waziri wa Maji Mheshimiwa Jumaa Aweso na Naibu wake Mheshimiwa *Eng.* Kundo Andrea Mathew kwa uchapa kazi wao mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ya Iroba iliyo Kata ya Bumbire na huu wa Makongora uliopo Kata ya Ruhanga, ilikuwa katika bajeti ya mwaka uliopita wa fedha, mwaka 2025/2026 lakini haikutekelezwa. Tunashukuru pia katika bajeti ya mwaka huu wa fedha 2026/2027 pia imewekwa. Pia, miradi hii inasubiri vibali vya Serikali ili zianze zile hatua za mwanzo za manunuzi, lakini baadaye kwenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kupata *commitment* ya Serikali kwamba, miradi hii itaanza kutekelezwa lini? Ninaporudi

kule jimboni niweze kuwapelekea wananchi habari nzuri na lile tabasamu ambalo ameliahidi Rais wa Jamhuri ya Muungo wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninatumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Adonis Alfred, Mbunge wa Muleba Kaskazini kwa kazi kubwa aliyoifanya, kwanza kabisa, kwa kusimamia na kufuatilia. Ninaona leo ameongea akiwa na tabasamu sana kwa sababu kulikuwa na mradi ambao ulianza mwaka 2021 na haukuwa umekamilika kwa miaka karibia minne. Sasa ndani ya uongozi wake amekuja kufuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tunavyoongea, mradi wa Kagoma umeshakamilika na Mheshimiwa Mbunge anaendelea kufurahia kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema, suala hili bahati nzuri tayari tumeshaliweka kwenye bajeti. Mheshimiwa Mbunge wiki iliyopita aliniletea barua ya maombi ya kuomba kibali kwa ajili ya kutangaza ule mradi. Bahati nzuri tulichokifanya ni kwamba, kwa sababu mradi ulikuwa na gharama kubwa, tulikubaliana kuvunja kuwa katika vipande vya awamu kwa awamu, na bahati nzuri Mheshimiwa Mbunge ametupa ushirikiano mzuri sana kwa sababu anafahamu mahitaji ya wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimpe taarifa nzuri Mheshimiwa Mbunge kwamba, Mheshimiwa Rais ameridhia tukaanze kwanza na Makongora, ambapo kibali tumeelekezwa tukitoe wiki ijayo ili mradi ukatangazwe na wananchi waanze kuona sasa kazi inaanza kufanyika pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi ukishakamilika, tunafahamu utaenda kusaidia wananchi zaidi ya 8,000. Ninaamini kabisa kwamba tutakuwa tumeokoa magonjwa ya mlipuko, tutakuwa tumeokoa magonjwa mbalimbali yanayotokana na matumizi ya

maji ambayo siyo salama. Tunaamini kwamba hiyo itakuwa kazi kubwa sana ambayo atakuwa ameifanya, na sisi Serikali tutaendelea kumpatia ushirikiano. Ninakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ninakushukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Maji. Tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Yannick Ikayo Ndoinyo, Mbunge wa Ngorongoro aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 119

Ujenzi wa Vituo vya Forodha Ngorongoro

MHE. YANNICK I. NDOINYO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kituo au vituo vya forodha maeneo ya mpakani katika Tarafa za Loliondo na Sale, Wilayani Ngorongoro?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Yannick Ikayo Ndoinyo, Mbunge wa Ngorongoro kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo kwa huduma za forodha katika maeneo ya mipakani, ikiwemo mpakani mwa Tarafa za Longido na Sale katika Wilaya ya Ngorongoro. Uwepo wa vituo hivyo unaweza kuharakisha biashara, kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato, na kuimarisha udhibiti wa biashara zinazovuka mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu huo, kuna vigezo mahususi ambavyo Serikali inazingatia kabla ya kuanzisha vituo vya forodha mipakani, ili kupunguza gharama za uendeshaji na kuhakikisha ufanisi wa vituo husika. Vigezo hivyo ni pamoja na hali halisi ya mpaka *(strategic nature* ya mpaka wenyewe*)*, idadi

ya watu kwenye mpaka husika, na idadi ya mizigo inayohudumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kwa kushirikiana na taasisi nyingine zinazohusika na usimamizi wa mipaka, itafanya tathmini ya mahitaji na kuanzisha vituo vya forodha mpakani kwa Tarafa za Longido na Sale katika Wilaya ya Ngorongoro, kwa kuzingatia vigezo husika nilivyoviainisha hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilika kwa tathmini na endapo itaonekana inafaa, Serikali itajumuisha mradi huo katika mpango wa bajeti kulingana na vipaumbele vya Taifa. Serikali pia itahakikisha kuwa huduma za forodha zinafikishwa karibu na wananchi pamoja na wafanyabiashara ili kuhakikisha biashara na kudhibiti biashara ya magendo. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yannick Ndoinyo.

MHE. YANNICK I. NDOINYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, na kwa kweli ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Ninafurahi kwa sababu Serikali imekiri kwamba, kuwa na vituo vya forodha mpakani kule Loliondo ina tija, inaongeza biashara, na inaongeza uchumi wa watu na Taifa. Kwa kukiri huko, ninamwomba Mheshimiwa Naibu Waziri kama yuko tayari kufuatana na mimi kwenda kufanya hiyo tathmini ya awali, ili kuhakikisha kwamba hiyo nia na dhamira njema ya Serikali inaonekana ili tuweze kuanzisha kituo hicho. Je, yuko tayari kufuatana na mimi twende tukakague? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MSHAMU A. MUNDE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Yannick anavyowapambania wananchi wake wa Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua Mheshimiwa Yannick alishawahi kuwa Diwani wa Kata ya Longido. Kwa hiyo,

analifahamu jimbo lake vizuri sana, lakini pia anafahamu fika shughuli za kijamii, kibiashara, na kiuchumi zinazofanyika kwenye Jimbo lake la Ngorongoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua pia kwamba, ziko shughuli ambazo zinafanyika pale hasa hasa siku za Jumatatu. Alinishirikisha Mheshimiwa Mbunge huyu kwamba pale kuna shughuli nyingi sana za kiuchumi zinazofanyika siku za Jumatatu, ambazo kwa tafsiri ya kawaida shughuli hizo zinaweza zikaisaidia sana Serikali kuongeza mapato na kutimiza azma ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Mwaka 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tumepata taarifa pia mwezi uliopita na ninadhani ni tarehe 25 ya mwezi wa Nane, Mheshimiwa Dkt. William Ruto, Rais wa Jamhuri ya Kenya, alitembelea eneo linaloongelewa upande wa Kenya, ambapo panaitwa Pusimoru na Eneo hilo upande wa kwetu ni Oloika. Kutembelea kwake kukasababisha uanzishwaji na urasimishwaji wa eneo la upande wa pili, kuwa ni eneo rasmi la kuvuka mpaka kuja upande wa Tanzania kupitia mpaka huo. Hiyo ni dalili ya kwamba wenzetu wameona kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini Mheshimiwa Waziri wa Fedha hatakataa nitakapomshauri na kumwomba ruhusa ya kuambatana na Mheshimiwa Yannick kwenda kutembelea eneo hilo ili kupata tathmini ya awali ya kuanzishwa kituo cha forodha hapo eneo linaloongelewa. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Fedha.

Tunaendelea Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Tinnar Andrew Chenge, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 120

Utozaji wa Riba ya Pango la Ardhi

MHE. TINNAR A. CHENGE aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali inatoza wananchi riba ya pango la ardhi kuanzia mwezi Januari hadi Juni, badala ya kuanza kutoza unapoanza mwaka mpya wa fedha wa Serikali?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Tinnar Andrew Chenge, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Simiyu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995, Toleo la 2023, inatambua kuwa ardhi ina thamani na thamani hiyo inapaswa kutambuliwa na kukaguliwa kwa kuzingatia aina ya matumizi, mahali eneo lilipo, kiwango cha uendelezaji wa eneo na uwepo wa miundombinu mbalimbali katika maeneo husika. Thamani ya ardhi hutumika kukadiria ada na tozo mbalimbali zinazohusika katika ukamilishaji na miamala ya ardhi, ikiwemo Kodi ya Pango ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kodi ya Pango ya Ardhi huanza kutozwa katika kipindi cha mwaka wa fedha wa Serikali, ambao huanza tarehe 1 mwezi Julai ya kila mwaka katika kipindi chote cha umiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria, mmiliki ana wajibu wa kulipa Kodi ya Pango ya Ardhi kwa hiari ndani ya kipindi cha miezi sita ya awali ya mwaka wa fedha, ili kuwezesha utekelezaji wa mipango ya Serikali kwa mwaka wa fedha husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kifungu cha 35 (11) cha Sheria ya Ardhi, Sura ya 113, kimeweka utaratibu kuwa, endapo kodi haitalipwa ndani ya kipindi cha miezi sita baada ya tarehe ambayo ilipaswa kulipwa, riba ya asilimia sifuri nukta tano kwa mwezi italipwa kwenye kiasi ambacho hakijalipwa hadi kitakapolipwa. Vilevile, baada ya kipindi cha miezi 12, riba hiyo itatozwa kwa kiwango cha asilimia moja kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za riba ya Kodi ya Pango ya Ardhi kuanza mwezi Januari na siyo mwanzoni mwa mwaka mpya wa fedha wa Serikali, ni kwa sababu kodi hiyo inapaswa kulipwa tarehe 1 Julai ya kila mwaka na sheria inatoa kipindi cha miezi sita tu kabla ya kuanza kutoza riba. Ninaomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tinnar Andrew Chenge.

MHE. TINNAR A. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwa kuwa hati ya umiliki wa ardhi inatamka kuwa, mmiliki atapaswa kulipa kodi ya pango la ardhi kwa mwaka tarehe 1 Julai ya kila mwaka, Kifungu Na. 35(1) cha Sheria ya Ardhi kinamtaka mmiliki kuzingatia Sheria ya *Public Finance Act* wakati anafanya malipo haya. Hakuna kipengele chochote kwenye hati ya ardhi kinachomwelekeza huyu mmiliki wala kifungu chochote kwenye *Sheria* ya *Public Finance Act* kinachomwelekeza kwamba atapaswa kulipa kodi hii kabla ya tarehe 1 Januari. Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusu mgongano huu wa hizi sheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuzingatia Kifungu Na. 35 (1) cha Sheria ya Ardhi pamoja na Sheria ya *Public Finance Act* ambayo ndiyo inasimamia ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, ambayo inatamka kwamba, mwaka wa fedha wa Serikali unaanza tarehe 1 Julai mpaka tarehe 30 Juni ya mwaka unaofuata, Sasa, ni kwa nini mmiliki aanze kutozwa kodi hiyo tarehe 1 Julai badala ya tarehe 30 Juni, ili kuendana na tafsiri sahihi ya mwaka wa fedha wa Serikali *(Fiscal Year)*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kifungu anachokinukuu Mheshimiwa Waziri katika majibu yake cha Na. 35(11) kinakinzana na kifungu hicho Na. 35(1) cha Sheria ya Ardhi, lakini kinakinzana

pia na Sheria ya *Public Finance Act*. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kwanza kumpongeza sana mama yangu Mheshimiwa Tinnar Andrew Chenge. Kwa kweli amekuwa mshauri na mfuatiliaji sana wa maboresho ambayo yanaendelea kufanyika katika sekta ya ardhi na anatusaidia mambo mengi, hususan mambo haya ya kisheria ambayo yanatuboreshea sisi utekelezaji wa sheria ambazo mpaka leo tunazitumia katika sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kwanza kueleza. Kodi ina sifa zake na kodi siyo mchango. Kodi ina ulazima wa kulipwa, lakini kodi inamtaja mtu wa kulipa na inataja muda wa kulipa. Kwa hiyo, katika kuweka utaratibu wa kulipwa kodi hii, ni lazima ijipambanue na ionekane kabisa kuna ulazima wa kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana katika Bunge hili, kwa busara kubwa ambayo limeitafsiri kodi hii likasema, kodi hii ni lazima ilipwe kwa wakati, ndiyo maana likatunga Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 iliyoeleza katika Ibara ile ya 35, ambayo ikasema kabisa kuwa, sheria hii inafuata *Finance Act*. Mheshimiwa yuko sahihi kabisa, lakini sheria huwa tunasoma kwa umoja wake au kwa ukubwa wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukienda kwenye Kifungu hicho cha 35(11) ndiyo kinaelekeza sasa kuwa inapaswa ulipe ndani ya miezi sita bila *penalty*. Ukipita miezi sita, ndiyo utaanza kutozwa *penalty*. Bahati mzuri sheria hii imefanyiwa maboresho katika Bunge hili hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani ni mwaka jana, 2025 ndiyo tulipunguza kiasi hiki cha riba mpaka kufikia sifuri nukta tano. Lengo lake ni kufanya angalau unafuu uwepo, lakini bado ulazima ule unaonekana. Usipofanya hivi, adhabu yake itakuwa

siyo adhabu katika maana ya kuwa, inakufanya tu u-*comply* na ile sheria iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hakuna mkinzano wa sheria iliyopo na *Finance Act* au sheria ya fedha ambayo ameitaja, ila tu inakwenda kuonyesha ulazima wa sheria hii kutekelezwa katika kipindi fulani. Bahati nzuri sheria hii imempa mamlaka Kamishna wa Ardhi ili aweze kusimamia makusanyo haya ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninapenda kujibu maswali yote mawili haya kuwa, kwanza hakuna mkinzano, lakini pili kuwa kitu hiki kinachofanyika kipo katika sheria na sheria hiyo ilipitishwa na Bunge hili, na sisi kama wasimamizi tunapenda kusimamia sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii, tutumie ile *principle* ya *two minutes principle* ya kusema, kama una jambo la ulazima ambalo unaweza kulifanya ndani ya dakika mbili kwa uharaka wake, anza kufanya muda huo huo usichelewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninawomba Watanzania wenzangu na Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tutumie dakika mbili hizi tulizonazo sasa hivi, ingia kwenye simu yako, ona kama unadaiwa kodi ya pango la ardhi, lipa sasa hivi ndani ya dakika mbili kwa sababu tarehe 30 ya mwezi Disemba ndiyo mwisho wa kulipa bila riba. Baada ya tarehe 30 tutatoza riba ya sifuri nukta tano katika kipindi cha mwezi mmoja na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali hayo kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Tunamalizia sasa na Wizara ya Madini kwa swali la Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando, Mbunge wa Kilindi. *(Makofi)*

Na. 121

Mkakati wa Ujenzi wa Ofisi ya Madini Wilaya ya Kilindi

MHE. SALEHE M. MHANDO aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga Ofisi ya Madini Wilayani Kilindi?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando, Mbunge wa Kilindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kulitaarifu Bunge lako kwamba, Wizara ya Madini ina jumla ya ofisi 30 zilizopo katika Mikoa ya Kimadini Tanzania Bara. Wizara itaendelea kuongeza ofisi katika maeneo mengine pindi itakapojiridhisha eneo husika kumeongezeka shughuli za kimadini kwa kiasi kikubwa, na hakuna ofisi ya madini iliyo karibu ambayo inaweza kutoa huduma katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa, Wilaya ya Kilindi inahudumiwa na Ofisi ya Afisa Madini Mkazi wa Tanga.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salehe Mhando.

MHE. SALEHE M. MHANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini pia ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mavunde, kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika Wizara hii ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninaomba kuuliza swali la nyongeza. Kutokana na kasi kubwa na ukuaji mkubwa wa shughuli za madini katika Wilaya yetu ya Kilindi; je, Wizara ipo tayari sasa kutupatia Afisa Migodi na

akaweza kutumia sehemu ya ofisi zetu katika jengo bora kabisa la halmashauri, ili kuweza kusimamia na kuweza kutoa huduma kwa wananchi wa wilaya ya Kilindi? *(Makofi)*

Hapa Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo amekuwa mstari wa mbele kufuatilia masuala ya madini kwenye jimbo lake na mara zote amekuwa akihitaji kuona huduma hizi zinazogezwa karibu.

Mheshimiwa Spika, kwa swali la Mheshimiwa Mbunge ninataka nimhakikishie kwamba Ofisi ya Afisa Madini Mkazi wa Tanga tutasogeza karibu huduma ili kuweza kuhudumia Wanakilindi, na ombi lake la kumpeleka Afisa Mgodi wa kusimamia pale, kama Serikali tumelichukua na tutaangalia namna ya kuweza kusogeza huduma hii kwa kuanza na maafisa wa kawaida na baadaye tutafikia hatua ya kuwa na Afisa Mgodi katika eneo hilo. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, ninakushukuru.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo na wageni tutawatangaza baada ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:

TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE

NDG. BARAKA I. LEONARD - KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 37 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2025, ninaomba kutoa taarifa kuwa shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Shughuli za Mkutano wa Nne wa Bunge sasa zimemalizika.

SPIKA: Ahsante.

Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD - KATIBU WA BUNGE:

HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

SPIKA: Sasa kwa heshima na taadhima ninamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hatua inayofuata. *(Makofi)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kutuwezesha kufikia hatua hii tukiwa na afya njema na uzima na tukiwa tunahitimisha shughuli zote zilizopangwa katika Mkutano wa Nne wa Bunge la Kumi na Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbele ya Bunge lako Tukufu, ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutuongoza vyema na kwa juhudi zake za kuwatumikia Wananchi wa Tanzania. Sisi sote ni mashahidi na tunaona jinsi anavyofanya kazi bila kuchoka katika kuleta maendeleo kwa Taifa hili na wananchi kwa ujumla. Kwa dhati ya moyo wangu, ninakiri kuwa uongozi wake unaendelea kuwa chachu ya matumaini kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumtakia afya njema, hekima na maono makubwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kutekeleza majukumu yake ya kuliongoza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika niungane na wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania wote kwa ujumla kumpongeza sana Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais na kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini uzoefu, uweledi na uzalendo wake vitakuwa chachu muhimu katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kuliongoza Taifa letu na kutekeleza kwa ufanisi majukumu ya

Serikali kwa manufaa ya Watanzania wote. Ninampongeza na kumtakia kila la heri Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumtakia kila la heri katika majukumu yake hayo. Mungu ampe hekima, afya, njema na nguvu katika kulitumikia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, ninatoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuiongoza vyema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Tunazidi kumwombea heri na busara anapoendelea kutekeleza majukumu yake na hakika uongozi wake thabiti umejidhihirisha kwa vitendo kutokana na mapinduzi makubwa ya kiuchumi na ya kimaendeleo aliyoyafanya huko Zanzibar, hakika mkasi unaongea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge hili Tukufu kwa ufanisi wakati wa kipindi chote cha Mkutano huu wa Nne. Tumewaona mkiongoza mijadala kwa umahiri mkubwa. Ninawapongeza sana Wenyeviti wa Kamati ambao pia wamekuwa chachu, kama unavyojua kazi zote zinazokuja hapa zinapitiwa na Kamati zako za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote na Kamati zote za Bunge kwa kazi yenu nzuri na michango yenye dhamira ya dhati ya kuboresha mipango na kazi zinazokusudiwa kutekelezwa na Serikali. Michango na maoni yenu yanaendelea kuthibitisha uimara wa Bunge katika kutekeleza wajibu wake wa Kikatiba wa kuishauri na kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Spika, hakika hili ni Bunge la Wananchi wa Tanzania na ni Bunge lililotumwa na linawafanyia kazi Watanzania waliowachagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu tulipohitimisha Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi na Tatu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya teuzi mbalimbali zikiwemo za Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa

Mikoa, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi na Wenyeviti wa Bodi mbalimbali pamoja na Mabalozi.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza viongozi wote walioteuliwa kushika nyadhifa hizo na kuwatakia kila la heri katika kutekeleza majukumu yao hayo mapya. Niwakumbushe viongozi wote walioteuliwa katika utendaji wa majukumu yao katika nafasi mbalimbali kuzingatia sheria, kanuni, miongozo, sera, vipaumbele na kuweka juhudi na jitihada katika kuyatekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwapa pole Watanzania wenzetu waliopoteza ndugu, jamaa, marafiki na wengine waliopata madhara mbalimbali kutokana na ajali za barabarani na matukio mengine. Tunamwomba Mungu awape subira waliopoteza ndugu, majeruhi wapone kwa haraka na kuwapa Marehemu wote pumziko la amani.

Mheshimiwa Spika, leo wakati tunahitimisha Shughuli za Mkutano wa Nne wa Bunge la Kumi na Tatu, tumefanikiwa kutekeleza masuala mbalimbali ikiwemo wajibu wa msingi wa kutunga sheria, kujibu maswali na hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge, kujadili na kupitisha Miswada ya Sheria ya Serikali pamoja na kujadili na kutoa maazimio mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, Maswali ya Msingi 121 na ya nyongeza 351 na Maswali 12 ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu yaliulizwa na kupatiwa majibu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Miswada, Bunge lako Tukufu la Mkutano huu limepokea Miswada mitano ambayo ilisomwa katika hatua mbalimbali. Baadhi ya Miswada ambayo imesomwa ni pamoja na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo kwa Mwaka 2026 ambao umesomwa kwa hatua zake zote; Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto ya Mwaka 2026 ambao umesomwa kwa hatua zake zote; Muswada wa Sheria ya Mkopo kwa Dhamana za Mali Zinazohamishika kwa Mwaka 2026 ambao umesomwa kwa hatua zake zote; Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026 ambao umesomwa kwa hatua zake

zote; na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 02 wa Mwaka 2026 ambao nao umesomwa kwa hatua zake zote.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Maazimio; kwa mujibu wa Kanuni ya 113(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025 na kwa kuzingatia wajibu wa Bunge, Bunge lako Tukufu lilipokea na kujadili Azimio moja kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani.

Mheshimiwa Spika, ninalipongeza Bunge lako Tukufu kwa kupitisha Azimio hilo na Serikali ipo tayari kwa utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Taarifa za Kamati kupitia Mkutano huu Bunge lako Tukufu limepokea na kujadili Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu. Nilihakikishie Bunge lako Tukufu, Serikali inaenda kufanyia kazi mapendekezo yote ya Kamati na itawasilisha Bungeni taarifa ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Hoja za Serikali, utakumbuka tarehe 28 Agosti, 2026 nilitoa hoja ya kuliomba Bunge lako Tukufu lithibitishe uteuzi wa Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara 50(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Kanuni ya 42 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025. Kwa mara nyingine ninampongeza sana Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu kwa kishindo na kuonesha imani kwa Wabunge na kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi pamoja na Mawaziri, tuko tayari kuhakikisha tunatekeleza maelekezo yake, na pia kutoa mrejesho wa kazi ambazo tutakuwa tumezifanyia utekelezaji na kumshauri kwa hekima.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo utakumbuka Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania wakati akilihutubia Bunge lako Tukufu, alibainisha dhamira yake ya dhati ya kukamilisha miradi yote ya kimkakati. Dhamira hiyo imedhihirishwa kwa kukamilika kwa baadhi ya miradi mikubwa ya kielelezo ambayo imefanyika hapa nchini. Mradi mmojawapo ambao umekamilika na kama ambavyo umeshuhudia, ni Mradi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme wa Mwalimu Julius Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika falsafa yake ya *Continuity and Change,* sambamba na hayo ya Bwawa la Mwalimu Nyerere, dhamira yake ya dhati ya kukamilisha miradi ya ujenzi wa miradi ya kielelezo, mfano wa ujenzi wa Mradi wa *SGR* kwa vipande vyote, sote tumeshuhudia hivi karibuni akizindua kipande cha kutoka Tabora hadi Kigoma. Ili kufanikisha azma hiyo, ninaelekeza Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na Shirika la Reli Tanzania waweke mkakati mahususi wa kuendeleza kutekeleza kwa kasi miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa umahususi, kipande cha Mwanza - Isaka, Isaka - Tabora, Tabora - Kigoma na Makutopora - Dodoma. Kipande cha Isaka - Mwanza kiko hatua nzuri huenda kuanzia sasa mpaka Disemba ikawa hatua ya ukamilishaji, tutabaki na kipande cha Isaka - Tabora na kipande cha Makutopora - Tabora ambavyo na vyenyewe viko katika hatua za utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaelekeze Wizara ya Fedha na Wizara ya Uchukuzi wakishirikiana na Shirika la Reli pamoja na wakandarasi waliopewa kazi ya kujenga vipande hivi wapambane usiku na mchana, ikiwezekana ifikapo 2030 Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM wa kutoka Mwanza, Mara, Shinyanga, Geita, Kagera waje Dodoma wakiwa wamepanda *SGR* ya kutoka Mwanza mpaka hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa uzoefu tulioupata kwenye vipande vingine na ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, hili ni jambo linalowezekana hata Wajumbe wa Rukwa, Katavi pamoja na Kigoma kwa kuanzia wanaweza wakaikamata reli pale Tabora wakaja hapa Dodoma. Wakishamaliza kuandaa utaratibu wa utekelezaji wake, nitakutana nao Wizara ya Fedha, Wizara ya Uchukuzi, wakandarasi pamoja na wale tuliowapatia jukumu la

kuhamasisha fedha za miradi hii. tukimbie ili mradi huu uweze kukamilika na kufungua uchumi.

Mheshimiwa Spika, sote ni mashahidi na wengi wetu hasa Waheshimiwa Wabunge tulihudhuria na kushuhudia hafla ya uzinduzi wa Kituo cha Kufua Umeme cha Julius Nyerere uliofanyika tarehe 22 Agosti, 2026 uliongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, nirejee kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kujitoa na kuhakikisha nchi yetu inasonga mbele katika kukamilisha utekelezaji wa mradi huu wa kimkakati. Huu siyo tu mradi wa kufua umeme, bali umeitambulisha Tanzania kwamba ni nchi inayoweza kusimamia maazimio yake, ni nchi inayoweza kusimamia mipango yake, na kutimiza mipango ambayo imejipangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunapozungumzia Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Julius Nyerere, tunayo masuala mengi ya kujivunia. Kituo hicho kama nilivyosema siyo tu cha kuzalisha umeme, bali ni mfumo mzima wa miundombinu unaohitajika ili kuweza kuzalisha umeme, kusafirisha umeme na kuupeleka kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, tayari miundombinu hiyo imekamilika na umeme unaingia kwenye gridi ya Taifa. Ndiyo maana mikoa ambayo haikuwahi kuwa kwenye gridi ya Taifa sasa inaingia kwenye gridi ya Taifa. Kituo hiki kina mitambo tisa yenye uwezo wa kuzalisha jumla ya megawati 2,115. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzalishaji huo umeongeza kwa kiwango kikubwa, uwezo wa Taifa wa kuzalisha umeme na kuimarisha uwezo wa gridi ya Taifa kukidhi mahitaji kutokana na ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais alipokea nchi mradi huu ukiwa takribani 33% tu. Sambamba na miradi mingine mikubwa, jambo ambalo lingeweza kukatisha tamaa kutokana na ukubwa wake, lakini hakuyumba na mpaka miradi hiyo yote imeweza kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kituo hiki cha kuzalisha umeme endelevu unaotegemea upatikanaji wa maji ya uhakika, kwa msingi huo

nielekeze Wizara pamoja na mikoa husika kushirikiana katika kusimamia utekelezaji wa maelekezo ya Serikali ya kuhifadhi mazingira vyanzo vya maji na matumizi endelevu ya rasilimali katika Bonde la Rufiji pamoja na vyanzo vingine vinavyopeleka maji katika Bwawa hilo la Mwalimu Nyerere. Sambamba na hatua hiyo, Wizara ya Nishati iendelee kutekeleza mpango wa kuongeza uwezo wa uzalishaji kwa kutumia mchanganyiko wa vyanzo mbalimbali vya nishati, ikiwa ni pamoja na maji, gesi asilia, jua, upepo, joto ardhi, makaa ya mawe na vyanzo vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia ninapokwenda kwenye hoja nyingine, nitumie nafasi hii kulielezea Bunge lako Tukufu Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote ambao hata Waheshimiwa Wabunge walileta hoja hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kutekeleza tangu Januari, 2026 Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote. Ninaomba Watanzania wote, na Waheshimiwa Wabunge tutofautishe Bima ya Afya pamoja na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)*.

Mheshimiwa Spika, Bima ya Afya kwa Wote siyo mpango wa *TASAF,* siyo Mfuko wa *TASAF*. Serikali inachofanya kwa sasa ni kuyasaidia yale makundi yasiyoweza kuchangia Bima ya Afya kwa Wote, lakini ili mpango huu uweze kutekelezwa, ni lazima Watanzania wote waingie kwenye mpango wa Bima ya Afya kwa Wote. Nchi ambazo zilijaribu kutaka kutumia mpango wa Bima ya Afya kwa Wote sawasawa na Mfuko wa *TASAF* mpango huo ulifeli. Ili tusifeli, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote tutambue kuwa hii siyo *TASAF,* bali ni mpango wa bima ambao unamtaka kila Mtanzania mwenye uwezo aweze kujiunga na Bima ya Afya kwa Wote ili tuweze kuwasaidia wale wasio na uwezo.

Mheshimiwa Spika, ninaikumbuka kauli ya Mheshimiwa Dkt. Yahya Nawanda, akiwa Mkuu wa Wilaya wa Iramba wakati ule alikuwa akitumia kauli ya jogoo mmoja, matibabu mwaka mzima. Maana yake ni kila Mtanzania atumie moja ya kipato alichonacho kuunga mkono Bima ya Afya ili tuwasaidie wale wasio na kipato na hiyo ndiyo dhana halisi ya Bima ya Afya. Bima ya Afya ni ya wote na kila Mtanzania ashiriki ili tuwasaidie wale

ambao hawana uwezo. Ninaomba Watanzania wenzangu tusichanganye kabisa Bima ya Afya na *TASAF* kwa kuwa *TASAF* ni mpango na ni Mfuko unaogusa tu wale wasiojiweza. Bima ya Afya ni kwa wote. Tukibadilisha Bima ya Afya ikawa *TASAF,* tutakuwa tunafuata uelekeo wa wale waliowahi kufeli kutekeleza mpango huo.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kusisitiza kuwa kadiri ya Watanzania wakavyoweza kuhamasika na kujiunga na Bima ya Afya kwa Wote, ndivyo bima yetu ya afya itakavyokuwa na ufanisi mkubwa na ndivyo itakavyoweza kuwasaidia Watanzania wenye shida nyingi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tayari imeshaweka zaidi shilingi bilioni 48 na tayari inatibu magonjwa ambayo Watanzania walio wengi hawawezi kujitibu ambayo yanapata ruzuku kuweza kutibiwa. Twendeni kwenye Bima ya Afya ili tuwasaidie Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, sekta ya madini imeendelea kuwa nguzo kuu ya uchumi wa Taifa letu na kuwa moja ya sekta kinara katika kuchangia pato la Taifa. Nitumie fursa hii kuipongeza sana Wizara ya Madini inayoongozwa na ndugu yetu, Mheshimiwa Anthony Mavunde kwa kusimamia vyema maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kufanya mageuzi kwenye sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina shaka mtakubaliana na mimi kwamba mafanikio katika sekta ya madini yametokana pia na mchango mkubwa wa wadau wa madini. Kipekee ninawapongeza pia wadau wote wa sekta ya madini kwa mchango wao mkubwa wanaoutoa kwenye kuchochea ukuaji wa uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii imekuwa moja ya sekta kinara inayochangia katika mapato ya Taifa. Licha ya wachimbaji wakubwa, mchango wa wachimbaji wadogo kwenye uzalishaji wa madini umekuwa ukiongezeka siku hadi siku. Hii ni kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mazingira wezeshi kwa Watanzania kunufaika na sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba bado zipo changamoto mbalimbali ambazo tumeendelea kushauriana na Wizara pamoja na Wizara ya Kisekta pamoja na Wizara ya Fedha, yakiwemo mambo yanayohusu tozo kwa wachimbaji wa madini na maeneo mbalimbali ambazo ziko juu ya zile ambazo zimeainishwa kwenye sheria, kwa kuwa nyingine zinaangukia ndani ya halmashauri zetu kama tozo za huduma zaidi ya kiwango kilichoainishwa kwenye Sheria ya Madini, yaani zaidi ya asilimia sifuri nukta mbili tano ya thamani ya madini. Kwa miongozo ya sheria ya fedha, huu ni ukiukwaji wa sheria.

Mheshimiwa Spika, nielekeze Wizara ya Madini pamoja na Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI wakae kwa haraka kuziangalia changamoto hizo ili kufanikisha ufanisi huu uendelezwe ambao umeshapatikana katika sekta hii ya madini.

Mheshimiwa Spika, pia, ninazo taarifa katika baadhi ya maeneo kwa kuwepo watu walioshikilia leseni nyingi kwa muda mrefu ambapo ni kinyume cha utekelezaji wa Sheria ya Madini ambayo inawataka waendeleze maeneo. Maeneo haya makubwa ya uchimbaji na leseni hizo nyingi zikishikiliwa na mtu mmoja bila kuendelezwa, inasababisha Watanzania kukosa nafasi za kufanya shughuli hizo za uchimbaji na hasa hasa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, ili kutatua changamoto hiyo, nielekeze Wizara ya Madini ichukue hatua za haraka, hatua kali kwa mujibu wa sheria. Hatua hizo ikiwa ni pamoja na kufuta vibali na leseni zinazoshikiliwa kwa muda mrefu ili leseni za aina hiyo wapewe Watanzania, vijana wa Kitanzania wanaohitaji maeneo ya kuchimba. Yeyote anayetaka leseni yake isifutwe, atimize masharti yaliyowekwa kwenye leseni, aiendeleze na awapatie nafasi vijana wa Kitanzania ya kufanya shughuli hizo za uchimbaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua ambazo nimezisema kwa wale watakaokiuka sheria hizo, Mheshimiwa Waziri, futeni vibali hivyo, gaweni upya maeneo hayo kwa wawekezaji, Watanzania, vijana wa Kitanzania, wachimbaji wadogo wadogo kama ambavyo katika maeneo mengi Mheshimiwa Rais alishachukua hatua hizo na kuwafutia leseni na kuchukua hatua ya kuwapa vijana wa Kitanzania waweze kuchimba katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi ambazo Mheshimiwa Rais alizichukua ndizo zilizoongeza mapato na ndizo ambazo zimechangia uchumi wa vijana wa Kitanzania na mpaka hata kule Katoro ikapatikana harusi ambayo imefanyikia kwenye helikopta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na haya, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania imetoa utabiri wa mwelekeo wa mvua za msimu wa vuli kwa mwaka 2026 kuanzia mwishoni mwa Septemba Oktoba hadi Desemba ambapo imebainisha uwepo wa hali ya El-Nino ambayo itaambatana na mvua kubwa.

Mheshimiwa Spika, mvua za vuli zinatarajiwa kuwa za juu ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi ya Ukanda wa Pwani, Kaskazini, Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki, Ukanda wa Ziwa Victoria pamoja na Kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma. Mvua hizo zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya Septemba na wiki ya kwanza ya Oktoba kwenye maeneo haya niliyoyataja.

Mheshimiwa Spika, hali ya vipindi vya mvua kubwa inaweza kuambatana na mafuriko na kusababisha madhara makubwa kiafya, kiuchumi, kijamii, upotevu wa mali na uharibifu wa miundombinu. Serikali inaendelea kuchukua hatua za tahadhari huku tukitoa maelekezo katika maeneo mbalimbali kuimarisha uharaka wa kuyaangalia, kuzingatia maeneo yanayoweza kupata mvua hizo na kusababishwa na mafuriko.

Mheshimiwa Spika, hatua hizo ni pamoja na kuimarisha Kamati za Maafa ziweze kukabiliana na madhara yanapojitokeza na vilevile kutenga fedha ili kuwezesha matengenezo ya dharura ya miundombinu na kuirejesha katika hali ya kawaida. Ikumbukwe kuwa kwa sasa fedha za mifuko ya maendeleo ya miundombinu

zinapelekwa moja kwa moja kwenye mifuko husika ili kuweza kuongeza ufanisi. Tayari nimeelekeza mamlaka husika kuchukua hatua stahiki ili kuweza kuzuia ama kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo hayo, ni pamoja na kuandaa mipango ya utekelezaji katika maeneo yao ili kuzingatia Mpango wa Taifa wa Dharura wa kukabiliana na madhara kama hayo ya El-Nino. Nielekeze tena Kamati za Maafa katika ngazi mbalimbali, pande zote, mikoa hadi Taifa, mikoa hadi vijiji, tujipange kikamilifu kukabiliana na changamoto ambazo zinaweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, maeneo yote hatarishi yatambuliwe mapema, tathmini za vihatarishi zifanyike na hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. Tuhakikishe kuwa vifaa vya uokoaji, huduma za dharura pamoja na mifumo ya mawasiliano vinakuwa katika hali ya utayari. Idara na taasisi zinazohusika na miundombinu na usafi wa mazingira zihakikishe barabara zinazopitika wakati wote, mitaro na makalavati yanaimarishwa na kusafishwa ili pasiwe na utaratibu ule wa kuziba mifereji ambapo mvua hata za kawaida huweza kuleta madhara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya maji, umeme na mawasiliano, nazo ziweke mipango ya kuzuia madhara yanayoweza kujitokeza kwa kuhakikisha uharibifu unaepukwa ili huduma hizo ziweze kuwa endelevu. Kwa upande mwingine, tunayo magari ya kuchimba mabwawa, yatumike kuweka miundombinu ya kudhibiti mafuriko yanayoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo maji yale yanasambaa kwa sababu hayana pa kwenda na tayari tuna magari ya kuchimba mabwawa. Tuyaelekeze katika maeneo ambayo tukichimba hayo mabwawa yatapunguza mtiririko ama kusambaa kwa maji yanayoweza kuleta mafuriko.

Mheshimiwa Spika, nitumie Bunge lako Tukufu kuwakumbusha wananchi wa Tanzania kuwa taarifa hizi za utabiri wa hali ya hewa zilizotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini

ni taarifa sahihi na tuzitumie kuchukua tahadhari ili tuweze kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Serikali inaendelea kuchukua hatua za kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa lengo la kuongeza ushiriki wao katika shughuli za uzalishaji na kupunguza umaskini hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wananchi wanashiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kuwa na uwezo wa kujikwamua kiuchumi, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kuimarisha usimamizi na uratibu wa mifuko, kuratibu na kusimamia uwezeshwaji wa wananchi katika vituo vya uwezeshaji, kuratibu na kusimamia masuala ya uendeshaji wa biashara hapa nchini, na kuweka utaratibu wa kutenga 30% ya zabuni za Serikali zote kwa ajili ya makundi maalum kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma kama sheria inavyotaka.

Mheshimiwa Spika, sasa tunaweka uratibu wa kushiriki Watanzania. Jana nilizindua kongamano, Watanzania washiriki katika shughuli za kiuchumi, uwekezaji na miradi ya kimkakati ili tuweze kujenga sekta binafsi inayoshikwa na Watanzania na hivyo kuzalisha ajira nyingi kwa vijana wa Kitanzania na mapato ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali imeendelea upya kutekeleza suala la mikopo kwa vijana na mikakati ya urejeshaji. Nitoe rai kwa Wizara na taasisi zinazohusika kuendelea kulitekeleza jambo hili kikamilifu na kwa ufanisi ili kama Mheshimiwa Rais alivyoelekeza na alivyotoa chachu ya fedha zaidi ya shilingi bilioni 200, Watanzania wanaohusika hasa vijana na wanawake na makundi maalum waweze kunufaika na malengo hayo ambayo kwa nia njema Mheshimiwa Rais ameanzisha na ameonesha kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, nikiwa ninaelekea kumaliza, ninaomba nitumie fursa hii kutoa maelekezo mahsusi. Katika ziara zangu mbalimbali nilizofanya kule mikoani, nimeona kama ilivyokuwa kwenye ziara za Mheshimiwa Rais alipofanya katika mikoa mbalimbali, wananchi wengi wana masuala yao mahsusi

yanayowagusa moja kwa moja. Masuala hayo yakiwa ni upatikanaji wa huduma za jamii, utatuzi wa migogoro, kero kwa wananchi kwa wakati, utatuzi wa kero za wananchi kwa wakati na masuala yanayohusiana na mrejesho wa hoja zinazowasilishwa katika ofisi za umma.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia fursa hii kusisitiza kwa Waheshimiwa Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, watendaji wote Serikalini, Wakuu wa Wilaya na watendaji wa halmashauri tufanye kwa vitendo na kutoa mrejesho pale tunapotatua kero za wananchi.

Mheshimiwa Spika, ziara za viongozi wakuu zisiwe mbadala wa utatuzi wa kero na utekelezaji wa shughuli za kila siku za Serikali. Tathmini iliyofanyika imebaini kuwa wananchi wengi wameendelea kuwasilisha kero zao moja kwa moja kwa viongozi wa Kitaifa. Huu siyo utaratibu wa kawaida. Tuna ofisi za Serikali mpaka ngazi ya kitongoji na mitaa. Haipaswi mwananchi wa kawaida kuhangaika kupeleka kero yake mpaka mkoani, mpaka Taifani wakati kuna mnyororo wa utendaji wa Kiserikali kwenye kila eneo.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, niwaelekeze tena watendaji wote Serikalini waweke utaratibu wa kuwasikiliza wananchi, kutatua kero zao na kutoa mrejesho. Aidha, kwa zile kero wanazoona haziwezi kutatuliwa katika ngazi husika, watendaji wa Serikali wenyewe wazipeleke katika ngazi zinazofuatia kwa utatuzi.

Mheshimiwa Spika, vilevile niwaelekeze watendaji wa Serikali kuendelea kuzingatia kikamilifu vipaumbele vilivyoainishwa katika bajeti zetu. Lengo ni kujenga uchumi himilivu kupitia mageuzi ya kidijitali, uwekezaji, na utekelezaji wa mikakati na sera endelevu za kibajeti ili tuweze kukuza uchumi. Vipaumbele hivyo ni kama ambavyo vilielezwa na Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Mipango, ikiwemo utawala, amani na usalama, uchumi imara na shindani, uwezo wa watu na maendeleo ya kijamii, uhifadhi wa mazingira, pamoja na sekta vichocheo vya kimageuzi.

Mheshimiwa Spika, hivyo ni jukumu la kila mtendaji kuhakikisha fedha zinazotengwa zinatekelezwa, zinaelekezwa katika miradi husika kwa wakati na kuleta tija. Ninasisitiza ubora wa miradi uendane na thamani halisi ya fedha. Niendelee kusisitiza haya kwa sababu katika baadhi ya maeneo tumeona ukiukwaji. Kwa kuzingatia hayo, hatua stahiki zichukuliwe kwa maeneo yenye fursa hizo ambazo maelekezo haya hayatazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza vipaumbele hivyo, Waziri wa Fedha alitoa rai kubana matumizi na kuelekeza fedha kwenye vipaumbele. Kwa kuzingatia hilo, ninaelekeza hatua zichukuliwe katika maeneo yenye fursa za kupunguza matumizi bila kuathiri ufanisi wa shughuli za Serikali. Maeneo haya ni pamoja na matumizi ya uendeshaji wa magari ya Serikali, matumizi ya shajara, gharama za safari za ndani na nje, gharama za michakato ya bajeti kwa kupunguza idadi ya watumishi wanaoshiriki, gharama za mikutano, warsha, makongamano pamoja na safari nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, bado tuna fursa ya kupunguza haya. Ninayo mifano. Nitatoa mfano mmoja. Ningali Mbunge, ninakumbuka nimewahi kuwa Mjumbe wa Kamati ya *LAAC*. Ikifika Bajeti ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wakurugenzi wote na *CMT* zote, Kamati za Fedha wote wanakuja nchi nzima. *CMT* ile ina watu kama 14 hivi, ukiweka na Wakurugenzi, ukiweka na Mkoa, maana yake ni kama mkoa mmoja wanakuja watu 100 mpaka 180. Kwa nchi nzima ni kama watu 5,500 mpaka 6,000.

Mheshimiwa Spika, wanaoingia pale kwenye chumba kile cha Kamati kuonana na Kamati ya Bunge, wanaoongea, wakiongea wengi ni watatu mpaka wanne. Wengine wote wanasubiria nje. Haya ni mambo ya mazoea ambayo tunaweza tukayaepuka, na fedha hizo tukazipeleka kwenye ujenzi wa madarasa ambayo yatahitajika sana tunapoanza utekelezaji mpya kwa mageuzi ya elimu. Hivyo ni vitu ambavyo tunaweza tukavipunguza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeshuhudia hata kwenye ziara, ni vitu vya mazoea, vimezoeleka. Unaenda kwenye Mkoa A ambapo

utaenda wilaya zote, lakini kwenye wilaya zote Watendaji wa Mkoa mzima, hata wilaya ambapo hutaenda, wote wako kila wilaya. Matokeo yake mnaenda kukagua darasa lililojengwa kwa shilingi milioni 24, lakini mnaenda na magari 150. Ndiyo hapo sasa gari la Mbunge linakuwa la 151. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, awaelekeze Wakuu wa Mikoa pamoja na idara mbalimbali, haya ni mambo tunaweza kuyaepuka. Wanaenda kwenye bajeti, wazimalize kule kule mikoani. Afisa Masuhuli ambaye ni Katibu Tawala na Mkuu wa Mkoa na Afisa Bajeti waende kukutana na Kamati. Mbona tukienda kukutana na *IMF, World Bank* unakuta wao wako wawili tu, ninyi mko 50. Wao wako wawili tu, tena kukutana na Balozi, unakutana na Balozi na Msaidizi wake. Ninyi mko 33, mnakaa upande wenu, mnazunguka mpaka na upande wao. Haya ni mambo ya mazoea tu.

Mheshimiwa Spika, kila Katibu Tawala wa Mkoa aisome bajeti ya mkoa wake, Mkuu wa Mkoa atafungua, atakaribishwa, atakaribisha wataalamu waliotoka mkoani kwake. Katibu Tawala na Afisa Bajeti wazisome bajeti wazielewe. Huu utaratibu wa kuleta watendaji wote nchi nzima, wote! Halmashauri ziko 184, wakija na magari matatu matatu ni magari zaidi ya 500, yanatumia mafuta.

Mheshimiwa Spika, mkutano mmoja wa kuangalia bajeti, wanaoongea watu watatu tu zinatumika zaidi ya shilingi bilioni 20. Tunahitaji shilingi bilioni 20 tu kujenga madarasa yote haya tunayohitaji ili tuweze kukamilisha mageuzi katika elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye ziara hivyo hivyo, Mkuu wa Mkoa anatosha na wilaya husika kupokea. Wilaya zote zinaenda kumpokea! Wote! taasisi zote, wilaya zote, ofisi zinafungwa kwanza. Yakipita magari, ni kama wale nyumbu wanahama kutoka Tanzania wanaelekea Kenya. Nini? Ziara.

Mheshimiwa Spika, haya ni ya mazoea tu, tunaweza tukayabadilisha. Hasa hasa, siyo kwamba sipendi watu wasafiri, tuna jambo kubwa Ndugu Watanzania. Kuanzia 2028 tunatarajia watoto wanaokwenda kuanza *Form One* wawe mara tatu ya

wale wanaokwenda kuanza *Form One* kila mwaka. Walikuwa wakianza 900,000, sasa wanaenda kuanza zaidi ya milioni tatu.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji zaidi ya vyumba 8,000 vya maabara, tunahitaji zaidi ya vyumba 16,000 vya madarasa, na tunahitaji zaidi ya walimu 27,000. Lazima tubadili tabia ya matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusipobadili tabia ya matumizi, watoto wetu watarudi tena kusomea chini ya mti. Tusirudi huko, tulishavuka. Kwa hiyo, haya ni baadhi ya maeneo ambayo ninaamini kabisa tunaweza tukayarekebisha na wala yasiathiri shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, tunazo tozo mbalimbali katika halmashauri zetu na Serikali za Mitaa kwenye uzalishaji wa mazao yakiwemo madini, mifugo, na kilimo. Maelekezo yangu hayatofautiani na ya mwanzo. Tuzingatie sheria, na sheria inataka kama tunataka kuanzisha tozo mpya, tusiipitishe kabla hatujashirikisha Wizara ya Fedha ili kutokuanzisha tozo juu ya tozo nyingine na kuwapa mzigo mkubwa wananchi pamoja na wazalishaji wengine.

Mheshimiwa Spika, nilishukuru Bunge lako Tukufu kwa kuridhia kupitisha marekebisho yaliyokuwa yanapendekezwa katika baadhi ya maeneo yanayolenga kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Spika, tumebadilisha namna ya yaliyokuwa yamependekezwa marekebisho ya kuoanisha muda wa uongozi baina ya Meya na Naibu Meya sambamba na Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ili kuimarisha uwajibikaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, sasa patakuwa na uchaguzi wa mara moja kama ambavyo kwa Mwenyekiti miaka mitano, Makamu Mwenyekiti miaka mitano, Meya miaka mitano, Naibu Meya miaka mitano ili kuondoa fujo za watu kupanga makundi kila wakati na kuacha shughuli za kuwatumikia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna hatua za kumwajibisha yule anayefeli. Kwa nini tutumie kigezo kwamba tunaweza tukamchagua asiyefaa? Kwa hiyo, ili tuliepuke hilo, tuwe tunachagua kila mwaka. Tumchague aliye bora, lakini ikitokea tumemchagua asiyefaa, tumtoe, lakini tusifanye nchi nzima wako *busy* na uchaguzi kila mwaka. Katika hili, nilipongeze sana Bunge lako kwa kukubali pendekezo hili la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, limebaki jambo moja ambalo tulishalisema na hapa nimwelekeze Waziri wa TAMISEMI. Kila siku tunalia Wabunge kukosa vikao vya halmashauri. Kwa kuwa ratiba ya Bunge inafahamika, hata hapa kabla ya kutoa hoja nitataja kikao rasmi cha Bunge linalofuata, nitumie fursa hii pia kumwelekeza Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuandaa kalenda ya vikao vyote vya Madiwani na vifanyike wiki tatu kabla ya tarehe rasmi ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wiki tatu kabla ya Bunge, maana yake ni wiki moja kabla ya Kamati za Bunge. Kwa hiyo, vikao hivi vitafanyika hata kabla ya Kamati za Bunge kuanza kukaa. Lengo hili ni kutoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge ambao kisheria ni Madiwani, kushiriki pia vikao hivyo vya Madiwani kabla hawajaja kwenye Shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni wazi yapo maeneo mengine Wabunge wanakoseshwa vikao hivyo kwa makusudi. Hii siyo siri na wala siwasemi wote, ninawalenga wale wenye tabia hizo. Ukikuta Mkurugenzi ameshakuwa na Kabunge kake kale pale, ama anakaandaa ama wana dili zao tu, watapanga vikao ambavyo kwa vyovyote vile Mbunge atakosa tu kuwepo.

Mheshimiwa Spika, tumeweka kwenye sheria kwamba Wabunge ni Madiwani, lazima hizi sheria zitekelezwe. Kama tunaona Wabunge sio wa muhimu kwenye kukaa vikao vya Madiwani, tubadilishe sheria, lakini tusiwe kwenye sheria wanatakiwa wakae, halafu hawakai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kumwagiza Mheshimiwa Waziri apeleke hii kalenda, na kwa sababu tumeshaliongea, wakati ule tulitoa tamko na Bunge likiwa

linaendelea, kuanzia sasa atakayekiuka, huyo ni mkaidi na hastahili kuwa kwenye hiyo ofisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa upande wa michezo. Serikali inaendelea kukamilisha maandalizi ya *AFCON* kwa mwaka 2027. Nitumie nafasi hii kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, kazi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu inaendelea kwa kasi kubwa. Miundombinu hiyo ni pamoja na ile ya viwanja vya mazoezi, viwanja vya mashindano, barabara za kutoka na kuingia viwanjani na kadhalika kuhakikisha uwepo wa huduma za afya, maji, umeme pamoja na miundombinu mingine wezeshi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa viwanja, Serikali inaendelea kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Jiji la Arusha, ambao umeshazidi 91%, na mradi wa ujenzi wa uwanja wenye uwezo wa zaidi ya watu 32,000 na kwa upande wa Zanzibar, Uwanja wa Fumba ambao na wenyewe uko katika hali nzuri. Kwa upande wa Dar es Salaam, ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa pamoja na viwanja vya mazoezi vya Gymkhana, Meja Jenerali Isamuhyo, na Shule ya Sheria tayari vimekamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Zanzibar mbali na Uwanja wa Fumba, upo pia Uwanja wa *New Amaan Complex Annex One* pamoja na *Annex Two* ambavyo vyenyewe vimeshakamilika na Uwanja wa Amaan ambao na wenyewe uko katika hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wasimamizi wa miradi, nisisitize thamani ya miradi iweze kuonekana *(value for money)* katika miradi hiyo. Kutokana na umuhimu wa michezo hii ya *AFCON* kiuchumi, nizielekeze Wizara na taasisi zinazohusika, kuendelea kuratibu namna ambavyo Tanzania itanufaika na kuwa mwenyeji wa mashindano haya. Wadau wote hakikisheni wanashiriki na pasiwe mkwamo ambao utapunguza ufanisi ama manufaa ambayo Tanzania ingeweza kupata kutokana na kuwa mwenyeji.

Mheshimiwa Spika, sisi ni wenyeji wa mashindano, hivyo tunapenda kuona Timu ya Taifa pia inakuwa na ubora na siyo

msindikizaji. Nitoe wito kwa walimu pamoja na *federation*, benchi la ufundi, kufanya jitihada za kuhakikisha kwamba kuanzia sasa tunaanza kuangalia kwa macho mawili mikakati ambayo itatuwezesha timu yetu iweze kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninajua *weekend* hii, timu zetu ngazi ya vilabu zinaanza kurusha karata zao katika Mashindano ya *CAF*. Simba, Yanga, Azam na Singida, ni wawakilishi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nitumie jukwaa hili, yaani Bunge lako Tukufu kuzitakia kila la heri timu zetu na kuwaomba Watanzania kwenye mashindano ya Kimataifa tuache ule ushabiki wetu, tutangulize Bendera ya Taifa mbele ili tuweze kuhakikisha kwamba wote tunaziunga mkono timu zinazoshiriki mashindano ya Kimataifa ili ziweze kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yanapofika mashindano ya Kimataifa, mimi ni shabiki wa Simba, na huwa ninapenda wanavyofanya. Kwa hiyo, nitoe rai hata wewe ushabikie ile timu nyingine ili tujenge uzalendo wa kuziunga mkono timu zetu zote za Tanzania ili ziweze kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nihitimishe hotuba yangu kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri; Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye amefanya kazi nzuri sana ya kutusaidia Wizara zote usiku na mchana. Katibu Mkuu Kiongozi ambaye amefanya kazi nzuri sana ya kuratibu na kusaidia shughuli hizi ambazo zinakuja hapa Bungeni. Wakuu wa Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama, Mkuu wa Mhimili wa Mahakama na taasisi nyingine zote ambazo tumekuwa nazo bega kwa bega katika kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kipekee nimpongeze Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard na wasaidizi wake wote, watumishi wote wa Bunge kwa huduma nzuri pamoja na msaada mkubwa wanaotupatia katika kipindi chote tunapokuwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudie tena kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Hamza Saidi Johari. Mwanasheria

Mkuu wa Serikali amekuwa mwepesi sana Wizara au Idara za Serikali tunapokuwa na jambo linapohitaji ushauri wa Serikali. Tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kadhalika, nirejee kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote. Tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, hoja zao zote ambazo walizitoa tutaendelea kuzifanyia kazi ili tuweze kuhakikisha kwamba yale ambayo wananchi wa Tanzania waliwatuma, wanapata matokeo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, niendelee tena kuwaomba wananchi wa Tanzania kuendelea kuungana na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhimiza umuhimu wa amani, ushirikiano na umoja wetu wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Rais amesema mara kadhaa, bila amani, utulivu, mshikamano na umoja wa Kitaifa, haya yote tunayoyapanga yakiwemo ya Kiserikali, yakiwemo ya sekta binafsi, yakiwemo ya mtu mmoja mmoja, hayataweza kufanikiwa. Jambo hili siyo la Serikali pekee, ni jambo la nchi nzima, na ni jambo la kila Mtanzania. Tuungane pamoja, tumuunge mkono Mheshimiwa Rais kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa ya amani, umoja, mshikamano na utulivu ili tuweze kutekeleza mipango hii ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inapiga hatua kubwa na siri moja ya mafanikio ni hiyo. Niwashukuru pia viongozi wote wa sekta binafsi, viongozi wote wa dini ambao wamekuwa nasi bega kwa bega katika shughuli hizi za maendeleo. Sekta binafsi ni chachu kubwa ya maendeleo na viongozi wa dini ni sehemu ya chachu kubwa ya wadau tunaoshirikiana nao kuhakikisha nchi yetu inaendelea kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninapenda kutoa hoja kuwa, Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi Jumanne, tarehe 27 Oktoba, 2026 saa tatu kamili asubuhi litakapokutana tena hapa katika Ukumbi wa Bunge Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

SPIKA: Hoja hiyo imeungwa mkono.

Waheshimiwa, kaeni.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Bunge kuahirishwa mpaka tarehe 27 Oktoba, 2026.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Hoja ya Kuahirishwa Bunge mpaka Tarehe 27 Oktoba, 2026 ilipitishwa na Bunge)

SPIKA: Walioafiki wameshinda, kwa hiyo, Bunge litarudi tarehe 27 Oktoba, 2026. *(Makofi)*

Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:

WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

(Hapa Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Ziliimbwa)

SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Huu wimbo wa pili watu wengi walikuwa wanatingisha midomo tu. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri yenye maelekezo na ninatumaini yatafuatiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu umezungumza jambo muhimu sana, suala la muunganisho wa *SGR* mpaka nchi za jirani. Hivi karibuni kulikuwa na kiongozi mmoja wa siasa, alikuwa

anawahadaa wananchi kwa kuwaambia kuwa hakuna mkakati wowote wa *SGR* kutoka Dodoma kwenda Tabora na wananchi wakawa wanapiga makofi. Kwa maana anawapotosha, anatoa taarifa ambazo siyo za ukweli.

Ninamshukuru Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Prof. Mbarawa, yeye aliliona hilo, naye akatolea taarifa. Ninataka wananchi mjue, nchi inakwenda kwa mikakati maalumu na mikakati iliyotimia. Kwa hiyo, hongera sana kwa kulisemea hilo. *(Makofi)*

Leo tulisema tutasoma tangazo la wageni baada ya Shughuli za Bunge kutokana na sababu maalumu. Sasa ni kipindi cha wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Nitaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika. Wapo wageni 15 wa Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, ni Maafisa Tarafa na Watendaji Kata kutoka Jimbo la Segerea, Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu George Anthony, Afisa Tarafa Ilala na Ndugu Heri William, Afisa Tarafa Ukonga. Karibuni. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Switbert Zacharia Mkama, Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambao ni Makatibu wa Mbunge, Jimbo la Ukerewe, mkoani Mwanza. *(Makofi)*

Wapo Wageni 89 wa Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, ni viongozi wa Halmashauri Kuu ya Dayosisi ya Mpwapwa mkoani Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima ambaye ni Ndugu Daniel Wambura, Mhazili kutoka Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Jijini Arusha. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali ambaye ni Ndugu Frank Mathayo, rafiki yake kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa ya Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Abubakar Alli Omari ambaye ni Ndugu Chambua Msanga, mfanyabiashara kutoka Wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni 105 wa Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, ni wanafunzi 94 na walimu tisa wa Shule ya Sekondari ya King'ori, kutoka Jijini Arusha. Karibuni. *(Makofi)*

Wengine ni wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Hawa ni Ndugu Jenifer Badi na Ndugu Irene Kimaro, ni wajasiriamali kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Taarifa ya Spika kuhusu mapendekezo ya kuongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa *(Monitoring and Evaluation)*.

Waheshimiwa Wabunge, Siku ya Jumatatu, tarehe 31 Agosti, 2026, Kamati ya Uongozi ilikutana kujadili na kuamua kuhusu uhitaji wa Bunge kuunda Kamati kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Dira na Mipango ya Maendeleo ya Taifa. Uundaji huo ulitokana na utafiti uliobainisha kwamba, sasa tunafanya uchambuzi na kujadili mapendekezo ya mpango, siyo utekelezaji wake. Kamati ya Bajeti imeshapitia mapendekezo ya mpango, na ufuatiliaji wake hufanyika kwa ngazi za kisekta.

Utaratibu huu umeonekana kuwa na upungufu ambapo suluhisho lake ni kuanzishwa kwa Kamati mpya ya Bunge. Kamati hiyo itakuwa mahsusi kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango ya Taifa kwa ngazi ya Kitaifa na kwa muktadha mtambuka.

Kama mnavyofahamu, Kamati ya Uongozi ndiyo yenye jukumu la kushauri kuhusu uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge kama ilivyofafanuliwa katika Fasili ya Pili, Kifungu Kidogo cha Tatu cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025.

Aidha, baada ya Kamati ya Uongozi kushauri kuhusu uhitaji wa kuanzisha Kamati hiyo mpya, niliitisha kikao cha Kamati ya Kanuni ili niweze kushauriana nao kuhusu suala hilo, kwa mujibu

wa Kanuni Fasili ya Tatu, Kifungu Kidogo cha Tatu (b) na (d) ya nyongeza ya Nane ya Kanuni.

Baada ya majadiliano, Kamati ilishauri Bunge kuunda Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ufuatiliaji wa Tathmini ya Utekelezaji Mipango ya Maendeleo ya Taifa. Ushauri huo wa Kamati ni kwa mujibu wa Kanuni ya 179(3) ya Kanuni za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati hii itaongozwa na Naibu Spika. Wajumbe wa Kamati watakuwa ni Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa ujumla. Kamati hii itakuwa na jukumu la kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Dira ya Taifa na Mpango wa Maendeleo ya Taifa. Msingi wa majukumu ya Kamati ni taarifa za Tume za Taifa za Mipango kuhusu Ufuatiliaji na Tathmini ya Mipango ya Taifa. Kwa mantiki hiyo, majukumu yake hayataingiliana na majukumu ya Kamati nyingine.

Kwa hali hiyo, Kamati ya Kanuni ilipitisha marekebisho ya kanuni katika nyongeza ya nane kwa kuiongeza Kamati ya Ufuatiliaji na Tathmini kuwa ni moja ya Kamati za Kudumu za Bunge za sekta mtambuka. Marekebisho haya ya nyongeza ya nane yamewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili aweze kutangaza katika Gazeti la Serikali kwa mujibu wa Kanuni 180(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Baada ya hatua hiyo kukamilika, tutachapisha na kugawa kwa Wabunge nakala za vitabu vya kanuni.

Waheshimiwa Wabunge, lengo kuu la Kamati hii ni kwenda sambamba na Serikali kuhakikisha Dira 2050 inapata mafanikio makubwa kwa kipindi cha kwanza hiki cha mwaka 2025 – 2030.

Waheshimiwa Wabunge, Taifa letu bila kuwa na uwekezaji mkubwa, hatutaweza kuhimili mahitaji ya Watanzania. Lazima tuseme ukweli. Leo nchi yetu *GDP* yake ni asilimia sita nukta moja, lakini mahitaji na *dependency* ya wananchi ni kubwa mno. Kwa maana hiyo, asilimia sita nukata moja haiwezi kutosha kutufikisha Dira 2050, lazima tuwe na *serious investment* nchini Tanzania. *(Makofi)*

Investment hii ndiyo itakayoibua na kusaidia ajira za vijana na Watanzania katika nchi yetu. Yule ambaye hataki uwekezaji wa kiwango hicho ni yule ambaye hataki vijana wa Tanzania wapate ajira kwenye nchi yetu. Niwatahadharishe, wako watu wanapinga uwekezaji kwa lugha za uongo za kusema Taifa linauzwa au nchi inauzwa. *(Makofi)*

Sisi wote ni wawekezaji. Ukiwa na bodaboda, ukimpa mtu akuendeshee, huo ni uwekezaji, umemwezesha mtu kupata ajira. Ukiwa na *tax*i, umempa mtu akuendeshee, wewe ni mwekezaji, umempa mwananchi anaendesha na yeye anapata ajira. Tukiongeza uwekezaji katika Taifa, tutaweza kufika 10% ya pato la Taifa na hiyo *GDP* ndiyo itakayotunyanyua. *(Makofi)*

Tuko na uwekezaji wa bandari hapa. Leo bandari, kabla ya uwekezaji mkubwa wa *DP World,* kontena kila mwaka zilikuwa ni kati ya 500,000 na 600,000. Leo *up to* jana, kontena ambazo zimeingia katika bandari yetu ni 1,380,000. Hizi ni fedha. *(Makofi)*

Kwa nini tumekuza bandari? Tumeikuza kwa sababu mashirika ya meli duniani wamepata *trust* ya kuwa Tanzania inataka maendeleo, ina mwekezaji ambaye anaweza ku-*deliver* kuhakikisha meli inaingia kwa muda na inatoka kwa muda. Uwekezaji huu kwenye bandari umepunguza muda wa kushughulikia meli kutoka masaa 300 mpaka masaa 28. Hii ni *achievement* kubwa sana ambayo tumeipata. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilitaka nieleze, tujue kabisa bila uwekezaji mkubwa pia ni changamoto. Nilikuwa ninasoma hapa ripoti ya *World Bank,* wanasema, "*Tanzania faces a large challenge of turning its economic growth into jobs and ensuring that the growth reaches households.*" Lazima, tuna *challenge* kubwa sana. Uchumi huu lazima u-*generate* ajira za watu. *Manufacturing, tourism, agro-processing and mineral processing all have potential to create employment, but they will not expand fast enough if private investment continues to lag behind public construction.*

Tukiendelea na tamaduni zetu sasa hivi za *tourism* na za madini, tunapata fedha, lakini *it is not enough,* lazima tuboreshe. Leo kuna nchi jirani wanaanza mkataba wa miaka 30 *concession*

kuikodisha bandari yao, kuingia ubia na wakishaanza juu na chini, bandari zao zina ubora, bandari yetu itakosa mizigo. Tukikosa mizigo, tutakosa kuhudumia wananchi. Taifa hili *by* mwaka 2030, idadi ya Watanzania itakuwa siyo chini ya milioni 72. Hawa wanataka kula, wanataka huduma za afya, hawa wanataka ajira.

Kwa hiyo, mimi ninawaomba sana wananchi, hakuna nchi itakayouzwa na mtu yeyote. Maneno kuwa Tanzania inauzwa, ni maneno ya watu wanaotaka nchi hii isiwe na ajira na vijana mtumike tu kwenye mambo ambayo siyo mazuri. Msikubali, msikubaliane kabisa na mambo hayo. Leo kwa mfano, *sulfur* inakwenda nchi ya jirani, bandari yetu inahemewa sababu mzigo ni mkubwa, sasa ile nchi inabidi ichukue *sulfur* yake kutoka nchi nyingine mbele ya nchi yetu. *(Makofi)*

Sasa maboresho yanayofanywa na bandari ambayo tunatumia fedha za ndani ni kuongeza *efficiency* na kuhakikisha mizigo yote inakuja hapa. Leo wana-e*xtend berths* nyingine ambazo zitaweza kuchukua meli za mita zaidi 300, viwanja vitatu vya mpira. Faida yake nini? Badala ya kuleta meli nne kuingia bandarini, itaingia meli hii moja, itashusha mizigo na mapato mengi yatakayopatikana, yarudi kwa wananchi.

Waheshimiwa Wabunge, kuna nchi inaomba leo kuweka *depot* yake ya mafuta nchini Tanzania. Mbona anatuamini sisi Watanzania kuweka *depot* yake hapa, lakini sisi, tunaogopa kuamini watu kuja kufanya biashara ndani ya eneo letu.

Tunahitaji fedha za Serikali, makusanyo ya Serikali yakaboreshe mishahara ya wananchi, yaboreshe pensheni za wastaafu wetu, zikaboreshe huduma za afya, zikaboreshe shughuli nyingine za elimu na makazi ya wananchi wetu.

Katika miradi mikubwa tusikope fedha, tutumie fedha za mtu mwenye uwekezaji, awekeze, mradi kanuni na taratibu za nchi zinafuatwa. Ninajua nayasema haya sasa, jioni utasikia, Zungu kauza nchi, Zungu kauza nchi. Semeni, *as long as* kazi inafanyika, matokeo yanaonekana, na Watanzania wanakuwa na raha kwenye nchi yao. *(Makofi)*

Kuna nchi hapa, ninashindwa kuelewa; imefukuza Waafrika katika nchi yao, na wote mnaijua. Nigeria imewachukua wote wataalamu wa kilimo. Leo wote wamekwenda Nigeria wanaisaidia Nigeria kukuza kilimo kwenye Taifa lao. Kwa hiyo, nilitaka kuwaeleza vizuri sana, ni muhimu sana tukajua umuhimu wa uwekezaji. Uwekezaji huu lazima kuwe na *trust* kati ya Serikali na mwekezaji. Kwa hiyo, lazima kutakuwa na baadhi ya sheria kubadilika kwa maslahi mapana ya nchi.

Mnaona mpaka leo *LNG* haijapita bado. Haijapita kwa sababu Serikali inataka kusimamia maslahi mapana ya wananchi, Serikali ipate fedha ambazo zitakwenda kutumika kwa wananchi. Wakimaliza majadiliano, watasaini, lakini Serikali lazima ijue wananchi wake watafaidika vipi? Tunataka uchumi wa gesi, uchumi wa mafuta uweze kwenda kwa wananchi.

Kuna nchi ya jirani, juzi Spika wao amekuja hapa kwenye Bunge. Wanataka kushirikiana na Taifa letu katika kutafuta mafuta katika eneo lao. Ninamshukuru sana *AG* ameshapitisha eneo hili kwa upande wetu, bado upande wa kwao, wakishapitisha, mpango utaanza. Yote hiyo ni kwa sababu ya nini? Kuaminiana. Ninataka Watanzania muiamini Serikali hii ya Mama Samia. Haitauza nchi hii, lakini tunataka kuongeza Uchumi. Tukiongeza Uchumi, tunaongeza ajira. Tuna vijana wengi hawana ajira. Ajira hazitapatikana Serikalini, ajira zitapatikana katika sekta binafsi tu. Ninaomba sana mlielewe hilo.

Baada ya maneno haya, Katibu kuna lolote lingine?

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE: Tangazo kuhusu Jarida la Bunge.

SPIKA: Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa Ofisi ya Bunge imeandaa Jarida la Bunge, Toleo la 13. Jarida hili linaeleza masuala mbalimbali ya Kibunge ikiwemo baadhi ya matukio yaliyojiri wakati wa Mkutano wa Tatu wa Bunge na matukio katika Mkutano huu wa Nne.

Jarida hilo limeshawekwa kwenye vishikwambi vyenu na mengine mtagawiwa. Jarida liko kama hivi. Jarida hili haliuzwi, ni bure. *(Makofi)*

Baada ya maneno hayo, ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka tarehe 27 Oktoba, 2026 saa 3.00 asubuhi.

(Saa 6.28 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 27 Oktoba, 2026 Saa Tatu Asubuhi)

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA